ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nane - Tarehe 02 Disemba, 2016

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria Nembo na pamoja ya mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar Nam.12 ya mwaka 2004 na Kutunga Sheria inayoweka masharti bora yanayohusiana na Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya mwaka 2016 na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba pia kuweka Mezani Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi Nam. 9 ya mwaka 1992 na kutunga Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar majukumu uwezo na mambo yanayohusiana na hayo, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Waziri wa Afya): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Mswada wa Marekebisho ya Sheria Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya mwaka 2006.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Muhtasari wa Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar Toleo la 2012.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 142

Kuanza kwa Ukaguzi wa Bidhaa kwa Mfumo wa PVoC

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko mnamo mwezi wa Agosti, 2016 wameanzisha ukaguzi wa bidhaa nje ya nchi *"Pre-export Verification of Conformity" (PVoC).*

(a) Je, ni changamoto gani zilizojitokeza tokea kuanza kwa ukaguzi huo.

(b) Wizara imechukua hatua gani kutatua changamoto hizo.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 142 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza ningependa kutoa maelezo mafupi kuhusu mfumo wa *PVoC.*

Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) ina mifumo mikuu miwili ya ukaguzi ubora wa bidhaa zinazoingizwa nchini:-

1. Mfumo wa Ukaguzi Ubora wa Bidhaa baada ya kufika nchini na kabla ya kuingizwa sokoni *"Destination Inspection (ID)"*

2. Mfumo wa Ukaguzi wa Ubora wa Bidhaa kabla ya kusafirishwa na kuingizwa nchini yaani *"Pre-export Verification of Conformity to Standards (PVoC)"*.

Kutokana na *ZBS* kukabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ukosefu wa maabara pamoja na wataalamu wa kutosha katika kufanya kazi za ukaguzi pamoja na upimaji wa bidhaa zote zinazozalishwa nchini na bidhaa zinazoingia kutoka nje ya nchi, Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kupitia *ZBS* imeamua kuanzisha mfuko wa Ukaguzi Ubora wa Bidhaa kutoka nje ya nchi kabla ya kusafirishwa na kuingizwa nchini kwa bidhaa zote zinazoingia Zanzibar, yaani *"Pre-export Verification of Conformity (PVoC)"*.

PVoC ni mfumo wa ukaguzi, uhakiki na uthibiti ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwamba zinakidhi matakwa ya viwango vya kitaifa au kimataifa kabla ya kuingizwa nchini. Mfumo huu unatumika katika nchi nyingi ulimwenguni kote kwa kukuza biashara pamoja na kuharakisha uondoaji wa makasha ya bidhaa salama na zenye ubora bandarini na hatimae kuwalinda watumiaji.

Mhe. Spika, baada ya taratibu za manunuzi kukamilika, Wizara kupitia *ZBS* iliwateua mawakala wafuatao kwa ajili ya kufanya shughuli za Ukaguzi wa Ubora wa bidhaa nje ya nchi.

Kwa upande wa vyombo vya moto vilivyotumika (magari) ambapo ukaguzi huu umeanza tarehe 01/08/2016, mawakala wafuatao wameteuliwa na *ZBS* kwa ajili ya kufanya shughuli za ukaguzi:-

❖ *East Africa Auto Services Ltd* (*EAA*) kwa magari yanayotoka Japan, Singapore, Hongokong na UK.
❖ Jabal Kilimangaro *Auto ELect. Mech* (*JKAEM*) kwa magari yanayotoka nchi za Falme za kiarabu.

Kwa upande wa bidhaa nyengine (*general goods*) zisizokuwa vyombo vya moto vilivyotumika (magari) ambapo ukaguzi huu umeanza tarehe 01/11/2016, mawakala wafuatao wameteuliwa na *ZBS* kwa ajili ya kufanya shughui za ukaguzi:

✓ *Societe Generale de Surveillance S.A, (SGS),* na
✓ *Bureau Veritas (BV)*

Mhe.Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa ningependa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Tokea kuanza kwa mfumo huu, changamoto zifuatazo zimejitokeza:

- Mashirikiano madogo kutoka taasisi nyengine za Serikali zinazofanya kazi bandarini.
- Uchache wa wakaguzi waliopo bandarini.
- Baadhi ya wamiliki wa gari kutofata utaratibu wa kufanya ukaguzi baada ya gari hizo kulipishwa gharama za ukaguzi, kwa yale magari yanayoingizwa nchini bila ya kukaguliwa yanakotoka.

- Muingiliano wa kazi za ukaguzi pamoja na majukumu mengine kutokana na uchache wa wafanyakazi wa *ZBS*.
- Vishawishi vya rushwa, vitisho kwa wakaguzi kutoka kwa baadhi ya mawakala wa forodha ambao hawataki kufuata taratibu.

(b) Hatua ambazo Wizara kupitia *ZBS* imezichukuwa kuzitatua changamoto hizo ni:-

- *ZBS* inaendelea kufanya mazungumzo na taasisi zote husika ili kujenga mashirikiano zaidi ya utendaji kazi bandarini.

- Maofisa wote wa kazi za Kitaalamu ambao wameidhinishwa kuwa wakaguzi, hupangiwa zamu maalum kwa ajili ya kufanya kazi za ukaguzi bandarini.

- Wakaguzi waliopo bandarini wanaendelea kusimamia maadili ya kazi kwa kutopokea rushwa na kuwaeleza taratibu husika za kufuata pamoja na kuhakikisha kuwa kila malipo yanayofanyika mteja hupatiwa risiti.

- *ZBS* imekuwa ikiandaa vipindi vya redio na televisheni, pamoja na mikutano mbali mbali pamoja na wadau ili kuwapa taaluma kuhusu masuala ya viwango na uthibiti ubora.

- *ZBS* imewasilisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma maombi ya mshahara na posho maalum la mazingira hatarishi na mazingira magumu ili kutoa motisha kwa watendaji na kulinda wataalamu ndani ya Taasisi.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa mfumo huo wa ukaguzi wa *PVoC* ni mfumo mpya. Je, Wizara imejipanga vipi kutoa taaluma kwa wafanyabiashara na wadau mbali mbali ili wapate kuelewa.

b) Tokea uanze utaratibu huu, je, ni kiasi gani ambacho Wizara imeingiza kupitia ukaguzi huu, ahsante.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, kuhusu swali (a) taaluma tumetoa ya kutosha, yaani tumefanya mikutano na wote wanaohusika hapa Zanzibar na tukafanya mikutano Pemba kwa wafanyabishara na wanaohusika pia zaidi ya mara mbili. Pia, tulitoa taaluma kwa vyombo vya Serikali, yaani watendaji wakiwemo Makatibu Wakuu na Wakuu wa Idara zinazojitegemea. Vile vile na watendaji wengine ambao wanahusika na shughuli hii wa Wizara nyengine mbali mbali, taaluma hiyo tumeitoa.

Mhe. Spika, kuhusu kiasi gani tumepokea, kiutaratibu hizi fedha tunazozilipa huwa tunaletewa baada ya kuwepo kipindi maalum, mpaka sasa hivi tumeanza juzi hatutoweza kutoa taarifa, lakini tutaleta taarifa kipidi kingine kwa maandishi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi kuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Katika majibu ya msingi ya Mhe. Waziri, alisema katika moja ya changamoto ni kukosa mashirikiano na taasisi nyengine bandarini, naomba nimuulize ni Taasisi gani zilizokuwa hazitaki kutoa mashirikiano, ningeomba tukazipata kwa majina.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Katika jibu langu nilisema kwamba kuna changamoto katika kutekeleza suala hili, mjue kwamba agizo hili linapingana na baadhi ya matakwa ya wafanyabiashara, kwa hivyo na vile vile kuna vyombo ambavyo vinasimamia suala hili.

Bandarini kuna vyombo kwa mfano kama Bodi ya Chakula ipo bandarini, kuna *ZRB*, kuna *TRA* na kuna vyombo vyengine Idara ya Bandari, kwa hivyo, wote hawa wanatakiwa washirikiane na chombo chetu, kwa sababu bidhaa zinazotakiwa zikaguliwe zinatakiwa zikaguliwe tangu kule, lakini wengi wanakimbia huwa hawapeleki vyombo vyao kukaguliwa kule nje, kwa hivyo, wanapendelea kukaguliwa hapa ndani. Tunavyosema hivi vyombo bado vyengine havishirikiani na chombo hiki kwamba, wanaruhusu wakati mwengine na wanawatia moyo wafanyabiashara kuja kulipia hapa ndani kuliko kulipia kule nje ambako wanatakiwa walipe.

Mhe. Hassan Hamis Hafidh: Mhe. Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumsifu na kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Msoko, kwa kujibu masuala yake kwa umakini, hii ni kuonyesha jinsi gani *how experienced she is.* Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri, najua kwamba mfumo huu wa *PVoC* ni mfumo unatakiwa sasa hivi ufanyike katika nchi yetu kwa wanachama wa Jumuiya ya *East Africa*, nchi nyingi kama Tanzania, Uganda na nchi nyengine zote zinafanya kama hivyo. Lakini *observations* zangu zinaonesha kwamba si kipindi kirefu nilikwenda mimi mwenyewe nchini Dubai nikagundua mambo yafuatayo:

Kwanza, hawa wanaofanya *inspection* hawafanyi *Inspection* kama inavyotakiwa kwa sababu wao wenyewe hawana utaalam la kwanza, la pili, nchi yetu inapata asilimia thalathini na asilimia sabiini anachukua mfanyaji *inspection*.

Sasa naomba kuuliza swali lakini pia Mhe. Spika, nimebaini kama kuna gari haikufanyiwa *inspection* kule Dubai…

Mhe. Spika: Mheshimiwa, naomba uulize swali.

Mhe. Hassan Hamis Hafidh: Sasa naomba kumwambia Mhe.Waziri, anaonaje *inspection* hizi wakati inawezekana kufanyika Zanzibar zisifanyike Zanzibar ili nchi yetu mapato yale asipate yule wa kule badala yake yaingie Zanzibar na tunahitaji pesa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Kama nilivyojibu katika swali la msingi lililoulizwa mwanzo lenye (a) na (b), nilisema kwamba kuna masharti ya kimfumo wa biashara ambayo hayo yanatulazimisha bidhaa zote zinazotoka nje lazima zikaguliwe nje ili ziweze kuingia, na mnaelewa kuna kipindi tulikuwa na matatizo na zaidi hapa kuna wafanyabiashara wanapeleka magari yao Tanzania Bara na magari yao wanapeleka nchi za nje ya Tanzania Bara. Kwa sababu ya masharti yanatakiwa lazima yakaguliwe huko yanakotoka ndio yanaweza kuingia katika soko la *East Africa*, hiyo tumefanya sio tu kwa sababu ya mapato lakini kuangalia jinsi wafanyabiashara wa Zanzibar waweze na wao kuingia katika soko lile.

Ni sawa tunaweza tukasema tutaendelea na utaratibu wa nyuma, kwa sababu hapo nyuma mimi binafsi wakati nipo Wizara ya Fedha nilipinga utaratibu huo wa *PVoC* kwa sababu niliona wafanyabiashara wa Zanzibar wakati huo walikuwa hawajawa tayari kuingia utaratibu huu wa *PVoC*, lakini sasa hivi wafanyabiashara wana uwezo wa kutosha na wana biashara nyingi na wanafanya biashara nzuri. Kwa hivyo, itakuwa si vizuri kupata vikwazo wakati wanapeleka bidhaa zao Tanzania Bara, Kenya, Uganda au Ruwanda wakapata vikwazo kwamba hawajafanyiwa *inspection*, ikiwa kule watalipa gharama

nyengine na kuna *fine* sasa hivi, itakuwa si vizuri na tutalaumiwa sisi SMZ kwamba tunaendelea kuwasababishia wafanyabiashara wapate hasara.

Ninachosema Mhe. Spika, ni kwamba tujifunze tuendelee na jambo hili, kwa sababu hii biashara ya Zanzibar hatutaki iishie Zanzibar, tunataka wafanyabiashara wa Zanzibar waingie kimataifa na kimataifa kuna sheria zake na sababu zake nyengine tunafanywa sisi ambao ni wajumbe lazima tuzifuate. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ni kweli tunapata mapato kidogo kwa sababu wao wenyewe wale wanaofanya *inspection* inabidi na wao gharama zao wawe nazo na kuna mambo mengine tulipata malalamiko na yeye mwenyewe Mhe. Mwakilishi, ameniambia na tukawaambia tunayafanyia kazi baadhi ya mambo.

Lakini kusema turudie utaratibu wa nyuma Mhe. Spika, kwa sasa hivi itakuwa si vizuri kwa sababu haitoathiri na itatuongezea mapato kwa kusema labda, lakini itaathiri biashara za wafanyabiashara wa Zanzibar hasa wale wanaopeleka magari Bara na bidhaa nyengine, kama mnavyojua Zanzibar ni *Transit Trade Area*, kama tunazungumza *Transit Trade* tujaribu kuona kwamba tunataka keki na mayai lazima yavunjwe.

Mhe. Spika, hiyo ndio hali.(*Makofi*)

Nam. 144

Kuongezwa Posho kwa Waandishi wa Habari za Mawio

Mhe. Yussuf Hassan Iddi – Aliuliza:-

Kwa kuwa Waandishi wa Habari za Mawio wanalipwa kulingana na habari wanazopeleka, lakini malipo hayo ni madogo kulingana na ukubwa na ugumu wa kuzipata habari zenyewe, wakati mwingine huzipata habari hizo vijijini.

Je, ni lini wizara itawaongezea posho waandishi wa habari za Mawio angalau warejeshe nauli zao wanazotumia wakiwa katika kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-
Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 144 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, mwandishi wa kujitegemea anatakiwa ajitegemee na afanye kazi kuliko hata yule aliyeajiriwa, kwa sababu malipo yanatolewa kutokana unavyojituma kutegemea uwezo na harakati zake mwenyewe. Kwa hivi sasa

shirika linalipa sh.3,500 kwa *story* moja, sasa uwezo ni wako kama utapata *story* 2 au 3 au zote kama zitakuwa na vigezo vinavyohitajika basi utalipwa zote.

(a) Mhe. Waziri, suala la kuwaongezea posho waandishi wa habari na Mawiyo, Wizara yangu litaliangalia na kulizingatia kutokana na kutegemeana na kuimarika kwa Shirika na kuengezeka kwa mapato yake.

(b) Siku hizi *ZBC* inafanya safari za kwenda vijijini takriban mara 4 kwa wiki, *radio* safari 2 na *TV* safari 2 ambazo waandishi wa kujitolea kushiriki na kwenda kutafuta stori kwa mujibu wa uwezo wao.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Habari na Utalii, naomba kuuliza swali moja lenye (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa fedha wanayolipa kwa *story* moja ya Mawiyo sh.3,500 imeshapitwa na wakati. Je, Wizara haioni ni vyema ikaongeza fedha hiyo angalau sh.5,000.

b) Kwa nini katika kipindi cha Mawiyo stori za Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi haziruki hewani.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari na Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Kutokana na mazingira ya sasa kwamba 3500 kwa kulipwa mfanyakazi kutokana na mazingira anayokwenda kutafuta stori nakiri kwamba ni kidogo. Lakini kama nilivyoeleza katika swala mama kwamba suala hili Wizara italiangalia kwa kina kutegemeana na kuongezeka kwa mapato ya Shirika na wafanyakazi hawa tutawaboresha na kuwaongezea posho hizi.

Naomba Mhe. Spika, Mjumbe arudie swali (b).

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Spika, nimeuliza kwa nini wizara imezifuta stori za Wabunge na Wawakilishi kuruka hewani katika kipindi cha Mawiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari na Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, naomba niendelee kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza kitoto (b).

> (b) Mhe. Spika, wizara haijafuta stori na vipindi ambavyo vilikuwa vinaendeshwa na Wawakilishi na Wabunge. Nimuombe Mhe. Mwakilishi sasa hivi Wizara ilisimamisha kidogo tu kwa matayarisho kuna *programme* maalum iliyotayarishwa kwa ajili ya Waheshimiwa wote, Mawaziri na hata Wawakilishi wa majimbo na wale wa Viti Maalum kuna mpango maalum ambao wamepangiwa waende kule na kueleza zile sera zao na utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi, kuna masikitiko kidogo kwa wafanyakazi wetu hasa wa redio kamba Waheshimiwa Wawakilishi wanapokuwa na *functions* zao ambazo wanatangaza sera zao na yale ambayo wameyatekeleza kwa kipindi hichi na wale wafanyakazi wa redio pia wawashirikishe zile taarifa ili ziruke hewani na sio tu katika sehemu ya televishen, ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza na naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa kujibu maswali yetu kwa vizuri, swali langu lipo kama ifuatavyo.

a) Je, Mhe. Naibu Waziri, anaelewa kwamba asilimia 60 ya wazalishaji wa vipindi na watangazaji katika redio na *ZBC* ni hawa waandishi ambao bado hawajaajiriwa.

b) Anaelewa kwamba hii bei ya 3500 imeanza tangu mwaka 2000 mpaka leo iko bei hiyo hiyo analielewa hilo na haoni basi angalau elfu kumi (10,000) ndio ingekuwa kiwango sahihi kwa wakati wa sasa.

Mhe. Waziri wa Habari na Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika.

a) Nataka nimthibitishie ukichukua kitakwimu kwa vyombo vyote vilivyokuwepo chini ya *ZBC* wafanyakazi wa kujitolea hawawezi kufika idadi ya asilimia 60. Lakini bado wapo wengi na Shirika linaendeleaa na jitihada za kuhakikisha wale wote wenye uwezo wa kuajiriwa wataajiriwa katika kipindi kifupi. Wale ambao wamekuwa

wakichukua kazi zao kupeleka sehemu nyingine na kupata posho tu pale *ZBC*, wao waendelee na kufanya kazi zao kama watu wa kujitolea na bado na sisi tunaendelea kuwathamini kwa zile nafasi wanazozipata za kutuletea stori.

b) Mhe. Spika, swali la (b), kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri, kwa umakini kabisa, tumekiri kwamba pesa hizi au malipo haya ni ya zamani na yanapaswa kufanyiwa marekebisho. Katika *scheme of service* ambayo tunaifanya, nilieleza juzi hapa kwamba mabadiliko hayo yapo lakini inategemea na upatikanaji wa fedha kwenye Shirika letu hili la *ZBC*, zitakapopatikana wataongezewa. Ahsante sana.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, katika kituo cha Pemba kuna upungufu wa wafanyakazi kama *editing* na wapiga picha, ambapo wafanyakazi hawa wanatakikana wapige picha na wa-*edit* . Je, wizara yako ina mpango gani wa kuliona tatizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari na Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nakiri kwamba katika kituo chetu cha Pemba kuna upungufu wa wafanyakazi kama alivyouliza Mheshimiwa. Wizara yetu kwa kuwa sasa hivi serikali imesitisha ajira, nimuombe Mhe. Mwakilishi na nimuhakikishie kwamba, pale ajira zitakapofunguliwa tutaliangalia kwa kina suala hili na kulipa umuhimu wake na tuweze kuwaajiri vijana hawa, kwani serikali inataka vijana wake wote wawe na ajira na wajiendeleze katika maisha yao. Ahsante.

Nam. 56

Hatua za Kudhibiti Uharibifu wa Mazingira Uroa

Mhe. Simai Mohamed Said – Aliuliza:-

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, awali ya yote kabla sijaomba swali langu lijibiwe ningependa kutoa taarifa kwa Baraza lako kwamba, tumepokea salamu za pongezi kutoka kwa Mhe. Raphael Chegeni Mwenyekiti wa Tawi la *CPA* kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Katibu wa Bunge Ndugu Thomas Kashilila, wamefurahi sana na wamesema na wao watakuwa tayari kuungana na sisi sote na tutashirikiana kwa pamoja.

Lakini pia salamu zimekuja kutoka kwa Malkia mwenyewe pamoja na Donald Trump, pamoja na Obama, na wanasema kwamba safari zitakuwa nyingi, kwa hiyo, Wawakilishi tujitayarishe kwenda masafa marefu, tumefurahi sana.(*Makofi*)

Baada ya yapo Mhe. Spika, naomba swali langu kwenye orodha ya kazi ya leo nijibiwe, ahsante sana.

Katika Shehia ya Uroa kuna Hoteli inayoitwa Samaki *Lodge* iliyoongeza eneo lake kuelekea ufukweni kinyume na utaratibu. Ujenzi huo umechafua sana mazingira kwa kuzidisha kasi ya maji wakati yanapojaa na kupelekea kufukuliwa kwa makaburi na maji kuzidi sana kuelekea nchi kavu.

Ujenzi huo pia unaikosesha sana Serikali mapato kwani eneo hilo liliozidishwa halilipiwi kodi ya namna yoyote ile. Na hatua mbali mbali zimechukuliwa na Serikali ya Mkoa, Mamlaka ya Kuhifadhi Mazingira Zanzibar, Idara ya Mazingira pamoja na Serikali Kuu ili kuliondoa eneo hilo lililozidishwa, lakini bado hazijazaa matunda na athari zake zinaendelea kuwepo.

Je, Serikali inachukuwa hatua gani zaidi kuhakikisha kuwa hatua za kisheria zinachukuliwa kudhibiti hali hiyo inayoiathiri sana jamii na Serikali kwa jumla.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, tarehe 12 Oktoba, 2015, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alifanya ziara ya ukaguzi katika Hoteli ya *Palumbo Reef Resort* ama Samaki *Lodge*. Madhumuni ya ziara hiyo ilikuwa ni kuangalia tatizo la ukuta uliojengwa pembezoni mwa ufukwe wa hoteli hiyo na athari za mmong'onyoko wa fukwe unaoendelea pembezoni mwa maeneo yaliopo jirani na hoteli hiyo. Kasi ya mmong'onyoko huo kwenye eneo hilo limeongezeka kutokana na kujengwa kwa ukuta huo na kupelekea kufukuka kwa baadhi ya makaburi yaliopo jirani ya eneo la hoteli hiyo.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, baada ya kuona hali halisi na kupata maelezo ya eneo hilo, aliagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (*ZEMA*) na Idara ya Mazingira zishirikiane na taasisi nyengine kwa ajili ya kuchunguza ukuta uliojengwa na kutoa mapendekezo yanayofaa kwa Serikali.

Mhe. Spika, ripoti ya uchunguzi wa kadhia hiyo tayari imeshawasilishwa wizarani kwangu kwa ajii ya kuipitia na kuifanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo husika.

Mhe. Simai Muhamed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuwa sisi katika majimbo ya Mkoa wa Kusini na Wilaya ya Kati tunafanya kazi kwa nguvu ya pamoja na wananchi wetu wapo katika pande zote mbili. Lakini suala hili limekuwa linapokea malalamiko katika Ofisi ya Mkoa pamoja na Wilaya yetu ya chama pamoja pia na mwakilishi wa jimbo husika ambae pia ni Mhe. Waziri wa Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Mhe. Gavu), naamini malalamiko haya yamekuwa yanapita kwa pande zote mbili kwa pamoja.

Mimi nimuulize Mhe. Waziri, je, atakuwa tayari kuambatana na mimi pamoja na Mwakilishi wa jimbo husika na viongozi wa Mkoa ili kwenda kulimaliza hili tatizo na kuondoa hizi kero na malalamiko na manung'uniko yaliyokuwepo kwa wananchi hawa hasa katika hichi kijiji husika. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, nipo tayari kufuatana na yeye na Mwakilishi wa jimbo husika pamoja na ile Kamati husika ambayo imefuatilia kadhia hii mpaka tuifikishe mwisho.Ahsante.

Mhe. Suleiman Farhan Khamis: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi hii ya kuuliza swali dogo, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuamka salama usalimini. Pia, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, nchi nyingi sasa hivi kila moja ina sera yake; nyengine zina Sera ya kuvuta bahari na nyengine zina Sera ya kufukia bahari. Katika eneo letu, yaani Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, katika Wizara ya Ardhi, Maji na Mazingira, inakuwa kila unapotaka kutoa ushauri wa eneo hili kwamba liwe *beach* au hili tufukie kila siku wana sera yao ya kusema kwamba tunadhibiti bahari.

a) Je, Zanzibar sera yake ni kuvuta bahari kuja ndani au ni kuifukia.

b) Je, pale wanaposema kwamba wanadhibiti bahari, maji ya bahari yatakapokuja kweli hasa kwa mtindo wake wa kibahari wana uwezo gani wa kuyazuia maji hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kawaida tunatumia wataalamu kufuatana na hali halisi ilivyo, utaalamu una mipaka yake, inapokuja kudra ya Mwenyezi Mungu ya kuleta maji anavyotaka, nadhani si Zanzibar tu wataalamu wa dunia yote wanaweza wakashindwa kwa hilo.

Mhe. Spika, iwapo kuna miradi ambayo inataka kufanywa, tunapeleka wataalam kuona hapa, aidha, bahari tuifanye hivi, ama hii tuiwache hapa. Inawezekana eneo moja likafanywa tofauti na eneo jengine, inaangaliwa *geography* ilivyo na hali ya wataalamu wetu wanashauri vipi. Kwa ujumla hatuna tofauti na wataalamu wanafanya kazi kuhakikisha kwamba mazingira hayaendelei kutuathiri Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa majibu yake mazuri na naomba niongezee kidogo tu.

Mhe. Spika, katika njia za udhibiti wa bahari kupanda juu inategemea eneo husika. Kwa mfano, unapozungumzia eneo la bahari iliyoingia ndani kwa maana ya bahari ya koko, maana yake udhibiti wake mzuri wa kitaalamu ni kuotesha mikoko mipya, kadri utakapokuwa unaotesha mikoko ndivyo utakavyokuwa unaizuia bahari isipande.

Lakini pili maeneo yale ambayo yana matumbawe au viumbe halisia vya bahari, unapoendelea kuvitoa maana yake kwamba unaizuia bahari isije juu, maeneo ambayo yana ufukwe mweupe, yaani mchanga, utakapokuwa unazuia watu wasichimbe, yaani unapokimbiza ile *erosion*, maana yake *automatically* unaizuia bahari isipande juu kwa kasi, na maeneo ambayo yana *coral* kwa maana kwamba majabali yenyewe kimaumbile bahari inakuwa haiwezi kupanda.

Mimi nadhani kwamba njia nzuri ya udhibiti wa bahari ni kuendana na ile *eco-system* na ule mfumo halisi wa uhalisia wa maumbile ya bahari na eneo husika. Hivyo, naomba nitoe wito kwa wananchi wetu wa Zanzibar maeneo ambayo yana koko tuendelee kutunza koko na tuendelee kupanda koko. Maeneo ambayo yana ufukwe mweupe wa mchanga, tuendelee kuulinda ufukwe ule kwa kutouchimba mchanga kwa shughuli za ujenzi, na maeneo ambayo yana *coral* na viumbe vyengine vya kibahari tuendelee kuvitunza kwa faida ya uzalishaji wa samaki, udhibiti wa bahari pamoja na mambo mengine yanayoathiri upandaji wa bahari.(*Makofi*)

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kutokana na maelezo mazuri ya Mawaziri wote wawili, tunawashukuru sana kwa ushauri wao mzuri na tutaufanyia kazi. Lakini sisi tukiwa kama wananchi tupo katika vijiji vyetu ambavyo hatuhusiki na masuala ya utoaji wa ardhi, wala ugawaji wa ardhi wakati wa ujengaji wa mahoteli. Wawekezaji wanapokuja Wizarani kwa ajili ya kutaka kujenga hizo hoteli zao, sijui kuna masharti gani ambayo wanapewa kwa kuweza kudhibiti zile hoteli zao na zile ramani za hoteli zao ili kutoweza kujenga zile kuta ambazo zinazuia yale maji ya bahari. Tukiangalia huku kwetu Nungwi masuala haya yanafanyika sana na kuna mahoteli ambayo yanajenga kuta hizo kila mara, wanajenga zikisha zinaanguka.

Je, Mhe. Waziri, ni hatua gani ambazo zinachukuliwa kwa hawa wawekezaji wanapokuja huko wizarani kutaka hizi hati za kujenga haya mahoteli na ni masharti gani ambayo kuwa mnawapa kutokana na shughuli zao hizi ambazo wanazotaka kuzifanya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kikawaida muwekezaji anaangalia eneo, anakubaliana na wale watu ambao wanatumia ile ardhi kisha anakuja serikalini kwa ajili ya ukodishwaji wa ardhi. Masharti anakuwa anapewa katika *lease* namna ya kuitumia ardhi ile. Lakini tatizo ambalo tunalipata na ndilo kama tulilolizungumzia hili la Uroa linahusiana. Wanakijiji ama wananchi wanakubaliana kinyemela huko kwa huko, jambo ambalo linatusababishia matatizo kidogo. Ukitaka kuchukua hatua hapa utakuta kuna wengine wapo upande wa yule na wengine wapo upande wa huku.

Mhe. Spika, niseme kwa ujumla kwamba masharti bora ya utumiaji wa ardhi ndiyo yaliyokuwa yanapewa nafasi. Changamoto tuliyonayo ni baadhi ya wananchi baada ya makubaliano yale yanafanywa makubaliano mengine na wananchi wa eneo husika.

Nam. 106

Haki za Walimu Waliofukuzwa Kazi

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:-

Kuna walimu ambao walisimamishwa mishahara yao kwa tuhuma ya vyeti vyao kuwa feki, lakini baada ya Serikali kufuatilia walionekana ni vyeti halali.

Je, haki yao waliokuwa hawakupewa Serikali inawafikiria vipi. Na baadhi yao wameshafariki, wameacha warithi wao.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo Mwakilishi wa Jimbo la Chambani, swali lake Nam. 106 kama ifuatavyo pamoja na marekebisho yaliyofanyika:-

Ningependa kusema kwamba walikuwepo baadhi ya walimu ambao wakati wa zoezi la marekebisho ya mishahara mipya walikuwa hawajamaliza masomo yao na walipotakiwa kueleza kuhusu sifa zao za mwisho za elimu, walitaja sifa ambazo kwa wakati ule walikuwa bado hawajazipata. Pia, kulikuwa na walimu ambao hawakuwasilisha vyeti halisi vya kumalizia masomo yao. Walimu hao walizuiliwa kwa muda kupata mshahara mpya mpaka hapo vyeti vyao vitakapohakikiwa. Baada ya kukamilika kwa uhakiki na kuwasilisha vyeti halisi walilipwa mishahara waliostahiki na kudai malimbikizo ya mishahara yao.

Ni kweli kuwa malipo ya malimbikizo ya mishahara yao ilichelewa sana. Hata hivyo, nina furaha kumuarifu Mhe. Mwakilishi, kuwa malimbikizo ya mishahara ya walimu hao imeanza kulipwa kwa awamu ya kwanza. Kwa mwezi wa Septemba 2016, Wizara imeshawalipa walimu 239 waliostaafu na kufariki jumla ya Tshs. 293,332,610/- kati ya hao walimu 139 wamelipwa Tshs. 188,371,300/- kwa skuli za Unguja na Tshs 104,961,310/= wamelipwa walimu 100 waliofariki na waliostaafu kwa skuli za Pemba. Mungu awalaze mahali pema peponi *Amin*.

Malipo hayo yataendelea kwa walimu wengine baada ya uhakiki kukamilika. Wizara inapenda kuwahakikishia walimu wote wenye malimbikizo ya madai ya mishahara yao kuwa haki yao haitopotea na italipwa kwa awamu baada ya uhakiki unaofanywa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri, ni lini uhakiki huo utamalizika na kulipwa hawa waliobakia.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa zoezi hili linahitaji umakini na utulivu wa kutosha, hatuwezi kusema lini, lakini kadri hatua zitakapokamilika wataendelea kulipwa. Uhakiki

huu unakwenda kwa awamu pengine wakipatikana baada ya kukamilika kwa walimu labda 200 watalipwa na huku uhakiki unakwenda mpaka zoezi hili litakapokamilika mwisho wake.

Nam. 111

Uajiri wa Walimu wa Sayansi katika Mkoa wa Kaskazini –P**emba**

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Mhe. Waziri, kwa kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna changamoto kubwa ya uhaba wa walimu wa masomo ya *Art* na Sayansi, kwa hivyo, hupelekea walimu wa masomo ya *Art* kusomesha masomo ya Sayansi bila ya kuwa na utaalamu huo.

Je, Mhe. Waziri, Wizara yako inalijua hilo na kama inajua ni hatua gani ambazo mmeanza kuzichukuwa ili kuweza kutatua changamoto hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Viwe Khamis Abdalla Mwakilishi wa nafasi za Wanawake, swali lake Nam. 111 kama ifuatavyo:-

Ni kweli Wizara ina changamoto ya uhaba wa walimu hasa wa Sayansi, hali hii inasababisha kuwepo kwa baadhi ya walimu wenye taaluma ya sanaa na wana uwezo wa kusomesha Sayansi kusomesha masomo hayo.

Mhe. Spika, Wizara yangu ya Elimu na Mafunzo ya Amali imechukua hatua mbali mbali katika kuhakikisha kuwa tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi.

i. Jumla ya walimu 600 wenye taaluma ya sanaa wanaosomesha sayansi walioko maskuli wamefanyiwa uhakiki na kuorodheshwa. Walimu hao wanapatiwa na wataendelea kupatiwa mafunzo ya kuwajengea maarifa na ujuzi wa kuweza kusomesha masomo ya Sayansi. Mafunzo hayo yameanza kutolewa kupitia mradi wa *Retooling Programme* unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *SUZA*. Aidha, semina na warsha za mafunzo kwa walimu wa masomo ya Sayansi yanaendelea kutolewa na idara ya mafunzo ya ualimu kupitia vituo vya walimu (*TC*). Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa walimu hao kupitia mradi utaotekelezwa kwa mashirikiano kati ya SMZ na Benki ya Dunia (*ZISP*).

ii. Wizara yangu imo katika hatua za mwisho kabisa za kuajiri walimu 106 wa masomo ya sayansi ili kupunguza uhaba wa walimu hao katika fani hizo.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ninashukuru Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri, swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa walimu hawa wanasomesha fani au taaluma ambayo hawajaisomea. Pamoja na kuwa wanasema kuwa sasa hivi wanawapa mafunzo ili kuweza kusomesha somo hili la Sayansi katika maskuli yetu. Je, kuna chochote ambacho wanawapatia inapofika mwisho wa mwezi, kwa sababu walimu wa masomo ya *Art* na masomo ya sayansi huwa wanapewa mshahara tofauti na walimu hawa.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kuwa mpaka sasa Wizara haijaweka utaratibu wa kuwapa motisha mahsusi walimu wanaosomesha hivyo. Lakini pia ifahamike kwamba ile fursa ya kupata kusomesha masomo haya pia ni sehemu ya *incentive* katika kujenga uwezo wa walimu. Isipokuwa ni kwamba huwa wanapata posho kiasi fulani wakati wakiwa katika mafunzo hayo ya kujengea uwezo.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri hasa pale alipotwambia kuna zoezi la uajiri wa walimu wa Sayansi, lakini uzoefu unaonesha baadhi ya walimu wanaopangiwa skuli za shamba kwa lengo la kuziba nafasi za uhaba huu wa walimu wa sayansi baada ya muda mfupi tu huwa wanaomba uhamisho na kurejea mijini na lile tatizo linarudi pale pale. Naomba nimuulize swali (a) na (b).

Je, ni mkakati gani wa Wizara katika kudhibiti tatizo hilo.

(b) Kwa kuwa huko nyuma walimu waliajiriwa wengi na walishaomba uhamisho na kurejea mijini, kwa tatizo hili hili la walimu wa sayansi, Wizara lini itafanya uhakiki wa walimu wa Sayansi na kugundua kwamba wako wengi mjini na kuwarejesha katika vituo vya shamba ambako nako pia kuna tatizo hili la uhaba wa walimu wa Sayansi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama tulivyosema kwamba sasa hivi Wizara inatathmini upya walimu wake wote katika kila skuli na pale ambapo itaonekana kwamba walimu katika skuli fulani ni wengi watahamishiwa sehemu yoyote Unguja na Pemba, si mashamba peke yake hata Pemba tutahamisha pale ambapo kutakuwa kuna haja ya kufanya

hivyo. Mhe. Spika, hili tumejipangana tunafanya kazi hiyo na kati ya hao walimu w Sayansi 106 wako ambao tutawahamishia moja kwa moja Pemba kwenda kufanya kazi na wako moja kwa moja tutawapoleka skuli za mashamba. Wale wengine ambao walioko sasa na wao pia tutawahamisha bila kujali anaishi wapi au anakaa wapi.

Kwa hivyo, nadhani suala hili katika awamu hii tumelivalia njuga na tunajaribu kugawa walimu kwa mizani sawa. Tusingependa hata kidogo kuona labda wilaya fulani imejengewa uwezo zaidi wa walimu kuliko wilaya nyengine. Tunataka kujenga usawa katika suala hili. Ahsante.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumuuliza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, kiasi cha mwezi mmoja na nusu kulikuwa na uhakiki wa walimu na wafanyakazi uliofanywa na Serikali katika Wizara yako. Je, ni nini tumegundua katika uhakiki ambao umefanyika hasa kwenye wafanyakazi hewa, ama walimu hewa na ni hasara gani iliyopatikana katika uhakiki huo.

Mhe.Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli uhakiki umefanyika katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, na ripoti inaendelea kuandaliwa, kwa hivyo, tusubiri ripoti itakapokamilika na itakapojadiliwa tutaweza kutupatia taarifa.

Nam. 70

Barabara Zilizojengwa kwa Kiwango cha Kifusi chini ya Mpango wa *Mivarf*

(Mheshimiwa Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 139

Kutumia Gari za SMZ wakati wa Usiku

Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliweka utaratibu mzuri wa matumizi ya gari za Serikali hasa nyakati za usiku kwa kuomba kibali maalum kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Je, utaratibu huu umeishia wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan Iddi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, swali lake Nam. 139 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu mzuri wa matumizi ya gari za Serikali baada ya saa za kazi umeelezwa katika kifungu namba 25 cha Sheria namba 13 ya mwaka 2004. Kifungu hichi kimepiga marufuku matumizi ya gari za Serikali baada ya saa za kazi bila ya kibali cha Katibu Mkuu wa taasisi husika ambapo kwa taasisi zinazojitegemea wakuu wahusika wa taasisi hizo ndio wenye kutoa kibali isipokuwa kwa makundi yafuatayo gari zao hizi zinakuwa zinatembea wakati wowote tu. Makundi yenyewe ni kama hayo yafuatayo:-

- Gari za vikosi vya Ulinzi na Usalama.
- Gari za kubebea wagonjwa na zimamoto.
- Gari zinazotumiwa na wateule wa Rais.
- Gari zinazotumiwa na viongozi wastaafu pamoja na Spika mstaafu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza swali dogo tu la nyongeza kama ifuatavyo. Je, Wizara imejipanga vipi ili kudhibiti matumizi mabaya ya gari za Serikali hasa nyakati za usiku.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, kama nilivyosema hivi sasa Serikali inaendelea kubana matumizi hasa katika matumizi yale ambayo si ya kawaida, na moja wapo ya matumizi hayo ni kuhakikisha kwamba gari zote zile ambazo si za wateule niliowataja hapa basi zile gari zinadhibitiwa na Katibu Mkuu kwa vile ndio *mas-ul* wa matumizi ya fedha za Wizara, basi pale ambapo litatokea tatizo hili nina imani kubwa sana wahusika watachukuliwa hatua za kisheria zinazohusika, lakini kwa hivi sasa tunaenda vizuri na Makatibu Wakuu wote mimi ninawapongeza pamoja na wahusika wengine, kwa kusimamia vizuri Sheria hii ya 2004.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na ninamshukuru Mhe. Waziri, kwa majibu yake mazuri.

a) Nilikuwa ninamuuliza Mhe. Waziri kwamba, kila kiongozi anapokuja katika madaraka nikimaanisha Rais huwa anakuja na mbinu zake za kudhibiti baadhi ya mambo ambayo mwenyewe hakuyapenda. Nilikuwa ninamuuliza Mhe. Waziri, kwamba, zamani Mawasiliano

ilikuwa na vifaa vyake *complete* kama nikisema *tanks* za mafuta na vitu vyengine ambavyo vyote vinatumika kwa ajili ya Serikali ili kudhibiti pengine mambo ya rushwa na wizi. Utaratibu ule kwa hivi sasa haupo, nilikuwa ninamuuliza Mhe.Waziri, utaratibu ule umeondoka kwa kugundua makosa gani ambayo yamefanya leo kila mtu anunue mafuta yake mkononi au tuweke vituo vya mafuta kila mtu anapotaka mwenyewe.

(b) Nilimuuliza Mheshimiwa kwamba, je, utaratibu kama ule ambao unaonekana ulikuwa unadhibiti na ulikuwa una *programme* zaidi ya kuweka mahesabu zaidi ya serikali unaweza ukarudi tena katika muda huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, yeye ni shahidi kwamba, ni karibuni tu hapa jana na juzi tulipitisha Mswada kuhusu matumizi ya fedha vile vile na manunuzi. Kutokana na mswada huu tumejipanga ili tuhakikishe kwamba tunafanya kazi kwa mujibu wa sheria na vile vile, matumizi sahihi na kuhakikisha kwamba tunaokoa mali za serikali na kupeleka vifaa vinavyotakiwa katika sehemu husika. Kwa hivyo, mimi ninamuomba tu astahmili, kwamba ni kweli kuwa kuna baadhi ya taratibu tumeziacha lakini ninamuhakikishia kwamba kupitia sheria tulizozipitisha hivi karibuni basi utaratibu ule tutaurejesha kama zamani na ushauri wake tunauchukua na tutaufanyia kazi.

Mhe. Spika: Waheshimiwa, naona maswali yamekwisha, kwa hivyo, kabla hatujaendelea naomba nitoe matangazo machache ambayo yapo. Naomba nianze na tangazo la kazi, Mhe. Ali Suleiman Ali, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari anawaomba wajumbe wa kamati yake baada ya kuahirisha kikao mkutane mara moja ukumbi namba 3.

Tangazo jengine ni la wageni naomba kwanza niwatambulishe viongozi kutoka serikali ya wanafunzi Chuo cha Biashara Dar-es-Salaam *CBE* jumla yao ni 4. Bwana Mussa P. Mwakitinta ambaye ni Waziri Mkuu, Theresia C. Semiono ambaye ni Waziri asiye kuwa na Wizara, Bwana Issac William Naibu Spika na Bwana Ruben Lameck Waziri wa Mikopo. Karibuni sana Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi), Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu ni Bibi Prama Bharwaj na Marion Moleh. Bibi Bharwaj anaendesha Kiwanda cha *Sunflag* huko Arusha na kina wafanyakazi 2500. Pia, anamiliki Kiwanda cha *Mantas International* ambacho kiko Ulaya,

muekezaji huyu yupo hapa Zanzibar kwa matembezi na kuangalia uwezekano wa kusaidia vikundi vya kinamama. Karibuni sana, *you are most welcome to the Zanzibar House of Representatives. (Makofi)*

Baada ya matangazo hayo Waheshimiwa Wajumbe, Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Hotuba ya Uwasilishaji wa Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako niwasilishe Azimio la kufanya Marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012.

Mhe. Spika, kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo kujadili suala hili muhimu la Kanuni za kuendesha shughuli zetu ndani ya Baraza. Aidha, nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii adhimu ili niweze kuwasilisha azimio hili na kuridhia marekebisho ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya uendeshaji mzuri zaidi wa vikao vyetu vya Baraza. Aidha, nikupongeze wewe Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti kwa namna mnavyosimamia vizuri shughuli zetu za Baraza.

Mhe. Spika, sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote walioshiriki katika hatua mbali mbali za marekebisho haya ya kanuni zetu, na shukurani maalum ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza. Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala na wajumbe wote waliohudhuria kwenye semina ya Wajumbe wa Baraza kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya kanuni hizi. Hoja ya mapendekezo waliyoyatoa yamesaidia sana katika kuziimarisha kanuni zetu kwa ajili ya uendeshaji mzuri wa shughuli za Baraza.

Mhe. Spika, Toleo la Baraza la Wawakilishi tulilonalo sasa zimetumika katika kuendesha shughuli zetu kwenye vikao vya Baraza na kamati zake kwa zaidi ya miaka minne. Tangu zilivyofanyiwa marekebisho kwa mara ya mwisho mwaka 2012. Kutonana na mabadiliko mbali mbali na uzoefu katika uendeshaji wa Mabunge hasa katika Mabunge ya nchi wanachama wa Jumuiya za Madola, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi imeona ipo haja ya kuleta mapendekezo na marekebisho haya ili

kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Baraza lenyewe kupitia kwenu Waheshimiwa Wajumbe ndio lenye mamlaka ya kutunga Kanuni za Baraza la Wawakilishi na kwa maana hiyo pia kuzifanyia marekebisho kanuni hizo kadri inavyohitajika.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kuwa nguvu ya kutunga kanuni hizi za Baraza inatokana na Katiba ya Zanzibar na hivyo kanuni hizi zina uzito mkubwa ukilinganisha na kanuni nyengine zinazotungwa kutokana na Baraza hili kutoa mamla kwa taasisi nyengine za serikali kutunga kanuni kwa mujibu wa sheria. Shughuli zetu zote za vikao vya Baraza na kamati zake kwa kiasi kikubwa zinategemea sana masharti ya Kanuni za Baraza na hivyo Wajumbe wote wa Baraza tuna wajibu mkubwa kuzielewa, kuziheshimu na kuzitekeleza Kanuni za Baraza la Wawakilishi ili kuimarisha utawala bora ndani ya chombo hiki muhimu cha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, yapo mambo muhimu ya msingi yaliyotufanya kuzingatia haja ya kuzifanyia marekebisho kanuni zetu za Baraza. Miongoni mwa mambo hayo ambayo yamezingatiwa kwa kina na Wajumbe wa Baraza ni kama ifuatavyo:

Mfumo na utaratibu wa kamati za kudumu na haja ya kuanzishwa Kamati ya Bajeti na kazi zake.

Mhe. Spika, mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni ya 9, 11 na 107(1)(a), ni kumfanya Naibu Spika, asiwe Mjumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza, isipokuwa ataendelea kuwa Mjumbe wa Kamati ya Uongozi na Shughuli za Baraza.

Mhe. Spika, marekebisho mengine yanapendekezwa kwenye Kanuni ya 107(5)(1) ili uongozi wa Kamati za Kudumu uzingatie jinsia. Hii maana yake ni kuwa jinsia itazingatiwa katika kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa kamati husika. Aidha, marekebisho ya Kanuni ya 107(2), 108(13), 119(1)(a) ni kwa ajili ya kuanzisha utaratibu wa Spika kushauriana na Wanadhimu wa vyama vyenye wajumbe kwenye Baraza wakati wa kuteuliwa wajumbe kwenye Kamati za Baraza. Utaratibu huu unatumika Kenya, Uganda, Zambia na Canada na unatoa fursa pana zaidi ya ushirikiano baina ya Spika na uongozi wa vyama vilivyomo ndani ya Baraza.

Mhe. Spika, rasimu hii ya marekebisho ya kanuni pia inapendekeza kuanzisha kamati mbili mpya, yaani Kamati ya Bajeti inayoonekana marekebisho yake ya kanuni yatakuwa 106(k) na Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Mashirika ya Umma na Hesabu za Serikali za Mitaa marekebisho ya Kanuni 106(j). Kamati ya Wenyeviti inafutwa marekebisho yake sasa yatakuwa Kanuni 106(k) na kazi zake zitafanywa na Kamati ya Bajeti kwa marekebisho ya Kanuni 117. Aidha, marekebisho ya Kanuni 33 na Kanuni ya 116 yanakusudia kulipa uwezo Baraza la Wawakilishi kupitisha Azimio la kuzibatilisha kanuni au sheria ndogo ndogo zinazotungwa na mawaziri au mamlaka nyenginezo endapo kanuni hizo au sheria hizo ndogo ndogo zinapingana na Katiba au sheria mama.

Suala jengine ni taratibu za upitishwaji wa miswada na bajeti, mfumo wa kudhibiti muda na utaratibu wa upigaji kura.

Mhe. Spika, hivi sasa kanuni zinatambua aina mbili za miswada ya sheria, aina hizo ni miswada ya serikali na miswada ya wajumbe. Marekebisho ya Kanuni ya 78 yanaanzisha aina mpya ya miswada itajuulikana kuwa ni Mswada wa Kamati. Marekebisho haya yanatoa fursa kwa Kamati za Kudumu za Baraza kuweza kuleta Miswada ya sheria kwenye Baraza lako tukufu. Mabunge ya Tanzania, Uganda na Afrika Kusini tayari yameanzisha na yanatumia utaratibu huo kwa kuwa na miswada ya kamati.

Kanuni nyengine zinazorekebishwa kutokana na kuanzishwa kwa Miswada ya Kamati ni Kanuni ya 81, 83,84,85,86,87,88,89 na Kanuni ya 90.

Mhe. Spika, kanuni zilivyo sasa zinaelekeza kwamba ili mjumbe aweze kuwasilisha mswada wa mjumbe ni lazima kwanza aombe ridhaa ya Baraza ili apate ruhusa ya kuwasilisha mswada wake. Mwelekeo wa Mabunge kadhaa hivi sasa ni kuondosha ulazima wa kumtaka mjumbe kuomba ridhaa kwanza kwa ajili ya kuwasilisha mswada wake. Bunge la Tanzania nalo pia limeshafuta utaratibu huo. Chini ya Kanuni ya 81, tunapendekeza marekebisho ya 81(1) ili Baraza la Wawakilishi la Zanzibar nalo liachane na utaratibu huu la kuomba ridhaa kwanza kabla ya mswada wa mjumbe.

Marekebisho ya Kanuni ya 92 yanapendekezwa ili kulipa Baraza fursa ya kutoa maoni kuhusu mwelekeo wa mpango wa Taifa mapema zaidi kuliko ilivyo sasa, na pia kuiwezesha Kamati ya Bajeti kushughulikia mwelekeo huu wa mpango wa Taifa kabla haujawasilishwa kwenye Baraza. Aidha, Kanuni ya 94 na Kanuni ya 95 zinapendekezwa kurekebishwa ili mkutano wa bajeti uanze mwezi wa Mei kwa mujibu wa kanuni badala ya June, na pia bajeti za wizara

mbali mbali zitangulie kwanza kuwasilishwa Barazani kabla ya Bajeti Kuu ya Serikali. Mfano, ni Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari limeanza kutumia utaratibu huo. Aidha, marekebisho ya Kanuni ya 87(3) ni kwa ajili ya kuzifanya kanuni zetu kutambua rasmi upigaji kura kwa njia ya sauti ya “ndio” au “sio” wakati wa Kamati ya Baraza Zima.

Eneo jengine ni uwezo na mamlaka ya Kamati za Baraza katika upitishaji wa bajeti.

Mhe. Spika, marekebisho ya Kanuni ya 98(3) yanatoa ufafanuzi kwamba kwenye Kamati ya Matumizi kila mjumbe anaruhusiwa kutoa hoja moja tu ya kupunguza kifungu fulani ili isiwe mjumbe mmoja huyo huyo anatoa hoja zote tatu zinazohusiana na kifungu fulani.

Kanuni ya 98(6)(b) inarekebishwa ili kufuta utaratibu wa kupunguza shilingi mia moja kutokana na kutoridhika na sera, badala yake unaanzishwa utaratibu mpya wa kupunguza kiasi fulani cha fedha kama ishara ya kutoridhika na jambo maalum lilojitokeza. Aidha, marekebisho ya kanuni yanafanywa kwa kuongeza kanuni mpya ya 98(8) kwa madhumuni ya kufafanua matokeo ya kupitishwa hoja ya kupunguza shilingi moja au kupunguza kiasi fulani cha fedha.

Eneo jengine la marekebisho Mhe. Spika, ni nidhamu kwenye Baraza na udhibiti wa mahudhurio ya wajumbe.

Marekebisho ya Kanuni ya 66 yanapendekezwa ili kuongeza kanuni mpya 66(2) ambayo inaanzisha Kanuni za Maadili kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Kanuni hizo za maadili zinafanywa kuwa ni nyongeza katika Kanuni za Baraza. Kiini cha Kanuni hizo za Maadili ni ile misingi saba ya *Nolan Principles* iliyochapishwa na Kamati ya Viwango *Committee on Standards in Public Life ya huko England mwaka 1995.* Misingi hiyo ni kutokuwa na ubinafsi, kuwa na uadilifu, kutokuwa na upendeleo, kuwa na uwajibikaji, uwazi, ukweli, uwaminifu na uongozi uliotukuka. Bunge la Uganda limeingiza misingi hiyo kwenye kanuni zao na imekuwa ndio Kanuni ya Maadili kwa ajili ya Wabunge wa Uganda. Inapendekezwa kwamba kanuni hizo za maadili ziingizwe kwenye Kanuni za Baraza hasa ikizingatiwa kwamba Kifungu cha 13 cha Sheria ya uwezo, fursa na kinga ya Baraza la Wawakilishi Nam. 4 ya 2007 inaelekeza kuwepo kwa Kanuni za Maadili kwa ajili ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, marekebisho ya Kanuni ya 74 na Kanuni ya 107(6) na Kanuni mpya 107(7) yanakusudia kuimarisha uwajibikaji wa wajumbe katika suala zima la mahudhurio ya wajumbe kwenye Baraza na kwenye kamati.

1. Kwanza wajumbe watatakiwa ku-sign orodha ya mahudhurio mara mbili kwa siku; asubuhi na jioni.

2. Mjumbe asiyehudhuria kikao cha Baraza au kamati hata kwa dharura isipokuwa kwa dharura maalum kama vile kwa kufiwa na Baba yake, Mama yake, mke, mume au mtoto au sababu nyengine itakayokubaliwa na Kamati ya Uongozi kama hakuhudhuria hatolipwa posho za kikao ambacho hakuhudhuria.

3. Mjumbe yeyote atakayehudhuria nusu siku ya kikao cha siku atalipwa nusu ya posho ya kikao cha siku kwa mujibu alivyohudhuria. Hii maana yake ikiwa umehudhuria asubuhi na *sign* umeweka asubuhi, jioni hukudhuria maana yake utakuwa ni nusu siku.

4. Mjumbe yeyote asiyehudhuria vikao bila ya ruhusa ya Spika au Mwenyekiti wa Kamati, basi mjumbe huyo atatangazwa kwenye Baraza kwamba ana tabia ya utoro na taarifa hiyo itapelekwa pia kwenye chama chake cha siasa na utaratibu huu unalingana na unatumika kwenye Bunge la Uganda. Msingi wake kwa wale ambao Waheshimiwa watakuwa hawahudhurii vikao vya kamati au vikao vya Baraza matokeo yake watatangazwa hadharani hapa kuwa wewe ni mtoro na chama chako kitajuilishwa.

Eneo jengine Mhe. Spika, ni ushirikishwaji wa wananchi katika mchakato wa bajeti, muda wa uwasilishwaji wa Rasimu ya Bajeti kwenye Baraza, nafasi ya wahusika (*Stakeholders*) na mazingatio ya bajeti katika kamati. Marekebisho yanapendekezwa kwa kuongeza Kanuni 92(4) ambayo inakusudia kuwezesha Kamati ya Bajeti kuweza kuwaalika wahusika kutoa maoni yao kuhusu mwelekeo wa mpango wa taifa na Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, mambo mengine kwa ujumla ni kama ifuatavyo:
Marekebisho ya Kanuni ya 59(9) yanakusudia kuimarisha utaratibu wa mjumbe kutangaza maslahi binafsi katika jambo linaloshughulikiwa na Baraza au Kamati na pia yanatekeleza maamrisho ya Katiba ya kumnyima haki ya kupiga kura katika jambo ambalo ana maslahi binafsi. Aidha, marekebisho haya yanaweza kuweka utaratibu wa Kamati ya Maadili na kinga za wajumbe kuweza kupokea malalamiko dhidi ya mjumbe yeyote atakayekiuka kanuni hii.

Na pia inaweka utaratibu wa Baraza kumuadhibu mjumbe anayevunja kanuni hii, maana yake mjumbe mwenye maslahi binafsi lazima atangaze hadharani na pia hatoweza kupiga kura katika hoja inayohusika. Pamoja na mambo hayo ya jumla pia kuna marekebisho yanayohusu makosa ya lugha, makosa ya uchapaji na marekebisho mengine mbali mbali yaliyojitokeza katika kanuni zetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kwa kuwa Kanuni za Baraza la Wawakilishi zimeweka misingi muhimu ya kuendesha shughuli za Baraza la Wawakilishi kwa kuzingatia taratibu za kibunge na kwa kufata mila na desturi za Zanzibar. Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 157 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Baraza limepewa mamlaka ya kuzifanyia marekebisho kanuni hizo za Baraza kila inapotokea haja ya kufanya hivyo ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji bora wa shughuli za Baraza. Na kwa kuwa mapendekezo ya marekebisho ya hizi yamejadiliwa na Wajumbe wa Baraza katika ngazi mbali mbali ikiwemo Kamati ya Uongozi na shughuli za Baraza, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na semina ya Wajumbe wote wa Baraza kuhusu mapendekezo ya marekebisho ya Kanuni hizi na marekebisho yaliyopendekezwa katika vikao hivyo kuingizwa katika waraka wa marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Baraza limepewa mamlaka ya kuzifanyia marekebisho kanuni hizo za Baraza kila inapotokea haja ya kufanya hivyo ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji bora wa shughuli za Baraza.

Na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 157 ya Kanuni za Baraza Mamlaka ya Baraza kufanya marekebisho ya kanuni yanapaswa kutekelezwa kwa Baraza kupitisha Azimio la kufanya marekebisho haya. Na kwa kuwa jadweli la marekebisho ya kanuni yanayokusudiwa kupitishwa na Baraza limewasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza hili ili kuridhiwa na wajumbe. Hivyo basi, Baraza la Wawakilishi linaadhimia kuridhia na kupitisha marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama marekebisho hayo yalivyowasilishwa kwa Wajumbe wa Baraza kwa kadri ya Baraza itakavyoona inafaa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, sina budi kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu wa rehema kwa kutujaalia kukutana tena katika Baraza lako tukufu, kwani hii neema ya Mwenyezi Mungu kutupa pumzi na afya njema ambayo tunajivunia.

Mhe. Spika, aidha, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuwasilisha maoni ya

Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu mapendekezo ya Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la 2012.

Mhe. Spika, pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kuona umuhimu wa kufanya marekebisho ya Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi ambazo ndio mwongozo wa shughuli zote za Baraza kwa Waheshimiwa Wajumbe pamoja na watendaji wake.

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza tena kwa kupata uteuzi wa Naibu Waziri, ambaye alitoka katika Kamati hii Mhe. Mihayo Juma N'hunga tunamuomba M/Mungu ampe afya njema na amuwezeshe kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Nchi.

Mhe.Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Wajumbe wapya walioteuliwa ndani ya Kamati yetu, ambao ni Mhe Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na Mhe Dkt. Sira Ubwa Mamboya. Kamati inawapokea na kuwakaribisha sana katika utekelezaji wa majukumu yao ndani ya Kamati hii, tunatarajia uwepo wao utaongeza ufanisi katika kazi za Kamati. (*Makofi*)

Mhe. Spika, Kamati yangu kwa kutumia Kanuni ya 157(3) imepitia na kujadili kwa kina marekebisho na mapendekezo ya Kanuni hizi za Baraza la Wawakilishi na kutoa ushauri wake kuhusu mapendekezo haya. Ni imani yangu kuwa kazi hii nzuri iliyofanywa; lengo lake ni kutoa marekebisho ambayo yatasaidia sana kujenga na kuboresha kazi zetu ambazo kwa muda mrefu zilipata changamoto kiutendaji.

Mhe. Spika, vifungu ambavyo vimefanyiwa marekebisho na kutolewa mapendekezo vimezingatiwa sana umuhimu wake katika Baraza na kutafuta ufanisi wa kiutendaji ili kukidhi dira na malengo ya Baraza katika kuhakikisha kuwa limekuwa ni chombo cha kidemokrasia chenye ufanisi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa watu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile napenda kuwashukuru Wajumbe wa kamati yangu kwa michango yao muhimu waliyoitoa wakati wa kupitia Kanuni hii ambayo imeweza kuchangia kwa kiasi kikubwa kuboresha mambo mbali mbali yaliyomo ndani ya Kanuni hii. Sasa naomba niwatambue, wajumbe waliounda kamati hii, kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Machano Othman Said — Mwenyekiti
2. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis — Makamu Mwenyekiti

3. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa Mjumbe
4. Mhe. Wanu Hafidh Ameir Mjumbe
5. Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Mjumbe
6. Mhe. Ali Khamis Bakar Mjumbe
7. Ndg. Rahma Kombo Mgeni Katibu; na
8. Ndg. Ali Alawy Ali Katibu

Mhe.Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo mbali mbali ambayo Kamati yetu imefanya, na pia naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambao tumeandaa na tayari Waheshimiwa Wajumbe mumeshapatiwa.

Mhe. Spika, Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala inapongeza sana juhudi zilizofanywa na viongozi na watendaji wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuomba katika marekebisho haya kuainishwa wazi wazi majukumu ya Katibu wa Kamati kwenye Kanuni kwa kuingiza kanuni mpya ya 107(9) ambapo kupitia Kanuni hii Waheshimiwa Wajumbe watapata kujua lengo na madhumuni ya Katibu wa Kamati kuwepo katika Kamati husika pamoja na majukumu yake kama yalivyoainishwa katika kanuni hii.

Mhe. Spika, aidha kamati yangu inapongeza sana marekebisho haya kwa kuongeza kanuni ya 107(10) ambayo imeainisha na kuweka utaratibu mzuri kwa Kamati za Baraza kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Bajeti iliyoidhinishwa katika kipindi chote cha kazi za Kamati kwa mwaka wa fedha.
Mhe. Spika, Katika sehemu ya tatu ya Kanuni hii inayohusu Uhalali Wa Shughuli Za Mikutano Na Vikao Vya Baraza, kanuni ya 74(3) kinarekebishwa kwa kuongezewa aya mpya ya "**c**" na kusomeka kama ifuatavyo:- "wajumbe watano wanaowakilisha Baraza katika Bunge la Jamhuri ya Muungano"**.** Aidha, aya ya "c" iliyopo sasa itasomeka kama "d".

Mhe.Spika, katika sehemu ya nane Masharti ya Jumla Kuhusu Miswada Na Utaratibu Wa Kutunga Sheria, kanuni ya 84(8) imerekebishwa na kusomeka kama ifuatavyo:-

*"*Wakati akiwasilisha maoni ya Kamati, Mwenyekiti au mjumbe mwengine yeyote anayewasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti, anaweza kutaja majina ya Wajumbe walio wachache ambao maoni yao yanapingana na maoni ya Wajumbe wengi wa Kamati endapo yatakuwepo."

Mhe. Spika, Kamati yangu kupitia kanuni hii, inakubaliana sana na fasili hiyo iliyoongezwa kutokana na kuonesha wazi ukomavu wa kidemokrasia ambao nchi yetu inajali na kuthamini mawazo ya kila mmoja katika kuitetea jamii yetu.

Mhe. Spika, katika sehemu ya tisa ya Kanuni hii inayohusu utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu Mambo Ya Fedha, kanuni ya 96(2) inarekebishwa na kusomeka kama ifuatavyo:-

> "Waziri anayehusika na uwasilishwaji wa hotuba ya makadirio ya Wizara yake, atawasilisha kwenye Baraza hotuba yake kwa ufupi kwa muda usiozidi saa moja na nusu..."

Aidha, Kamati yangu inaamini kwamba kanuni hii itasaidia sana kupunguza idadi ya wajumbe ambao hutoka nje ya mkutano wakati shughuli ya uwasilishwaji wa Hotuba ya Bajeti ya wizara husika inaendelea kutokana na muda mrefu wa uwasilishwaji wa Haotuba hiyo.

Mhe. Spika, Kamati yangu inashauri kupitia marekebisho ya kanuni ya 106 ambayo imetaja Kamati za kudumu, ni vyema Kamati ambazo hazina kazi za kila siku zitolewe kwenye Kamati za kudumu kwa kuwa wajumbe wa Kamati hizo kazi zao hutokea kwa wakati maalumu tofauti na Kamati nyengine za Kudumu. Hivyo, Wajumbe watakaohusika wataitishwa katika Kamati hizo pale tu itakapohitajika. Pia, Kamati inapendekeza kuwepo kwa tafsiri itakayotofautisha majukumu ya Kamati za kudumu na Kamati Teule.

Mhe. Spika, katika kusimamia haki na wajibu wa Wajumbe na Watumishi, Baraza la Wawakilishi limezingatia sana suala la jinsia na kuhakikisha kuwa majukumu yote kwa mujibu wa sheria na Katiba ya Zanzibar yanagawiwa kwa kuzingatia Jinsia**,** kama ambavyo marekebisho ya kanuni ya 109(6) yanavyoelekeza na kusomeka kama ifuatavyo:-

"Endapo itatokezea Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza wote ni wanaume, Wajumbe wanawake watateua wajumbe wawili miongoni mwao kuwa wajumbe wa Kamati ya Uongozi."

Mhe. Spika, Kamati yangu inashauri kuwa uteuzi uliotajwa katika kanuni ya 109(6) hapo juu, ufanywe kwa kuchaguliwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi na sio wajumbe wanawake wenyewe kufanya uteuzi huo.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine Kamati yangu inatoa pongezi katika Kanuni mpya ya 92(4) baada ya kuzingatia na kuona umuhimu wa kuishirikisha jamii kutoa maoni yao kuhusu mchakato wa Bajeti na kutoa nafasi kwa Wadau mbali mbali ambao kupitia Kamati ya Bajeti wataalikwa na kushirikishwa kuhusu Muelekeo wa Mpango wa Taifa wa Bajeti ya Serikali.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo machache nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa hekma na busara, nao waitumie fursa hii ili waweze kutumia uelewa wao kuchangia na kurekebisha Kanuni hii, kwa kutoa maoni yatakayosaidia kujenga na kuleta ufanisi wa kazi zetu na hatimaye kuipitisha kwa kupata ubora wa hali ya juu.

Mhe. Spika, Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Waheshimiwa Wajumbe naomba kabla sijaanza kuwaita wachangiaji nitoe tangazo linatoka kwa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Mhe. Machano Othman Said anawatangazia wajumbe wa kamati yake wakutane katika ukumbi wa kawaida wa kamati mara baada ya Baraza kuahirishwa.

Tangazo jengine ni mechi niliambiwa kwamba Waheshimiwa Wajumbe mnakumbushwa kwamba ile mechi kati ya Baraza la *Wawakilishi Sports Club* na *Kigamboni Veteran* itakuwa kesho Jumamosi saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Amani. Kwa hiyo, munahimizwa nyote muhudhurie lakini zaidi wanatakiwa wachezaji wafike mapema na mimepewa *list* hapa:

(1) Mhe. Jaku Hashim Ayoub
(2) Mhe. Abdalla Maulid Diwami
(3) Mhe. Ali Salum Haji
(4) Mhe. Miraji Khamis Mussa
(5) Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)
(6) Mhe. Mohd Mgaza Jecha
(7) Mhe. Mihayo Juma N'hunga
(8) Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira)
(9) Mhe. Hamza Hassan Juma
(10) Mhe. Suleiman Sarahan Said; na
(11) Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf

Baada ya tangazo hili Waheshimiwa sasa naomba nimwite Mhe. Wanu Hafidh Ameir kama mchangiaji wetu wa mwazo na Mhe. Shehe Hamad Mattar ajiandae.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima leo hii kukutana hapa ikiwa ni siku ya mwisho ya Baraza letu hili tukufu.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru wewe kwa nafasi hii ili na mimi nichangie katika kanuni hizi ambazo tunazifanyia marekebisho ambalo azimio lake limeshasomwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, baba yangu Mhe. Mohammed Aboud.

Mhe. Spika, imenibidi nisimame kwa kuwa tu tunarekebisha kanuni hizi na kanuni hizi zitatufaa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini pia zitawafaa watu wa *front benchers* kama watakuwa wamezizingatia.

Mhe. Spika, nimpongeze kwanza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na katika uwalishaji wake alisema kwamba nguvu ya kutunga, kurekebisha, kupendekeza na kufuta kanuni ni za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Lakini nilikuwa nataka kumwambia nguvu zile zile ambazo Mhe. Mohammed Abood amezitaja ndizo nguvu ambazo Baraza wanazo sio tu kurekebisha kanuni lakini hata katika kurekebisha miswada ambayo serikali inaleta. Sisi nguvu ambazo tunazo katika kurekebisha hizi kanuni ni nguvu zile zile ambazo tunazo katika kurekebisha miswada ambayo serikali inaleta.

Mhe. Spika, mimi sitakuwa na mengi nitakuwa na machache kwa sababu ni Mjumbe wa Kamati hii na katika kamati nimeshatoa michango yangu ya kutosha, na ndio maana Mhe. Waziri akaja na hotuba ambayo amekuja nayo pale. Kwa sababu tulikaa sote wawili baadhi ya mambo tukakubaliana lakini baadhi ya mambo ni lazima Mhe. Spika, kama Mjumbe wa Kamati kuyasisitiza ili Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wazingatie lakini na serikali nayo izingatie.

Mhe. Spika, kwa kuanzia nataka nianze na kanuni 61(2c) ambayo kanuni hii imewapa mamlaka ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuingia na vyombo vya kielektoniki pale wanapohisi inafaa kuingia navyo katika Baraza.

Niipongeze hatua hii Mhe. Spika, kwa sababu hivi sasa kila kitu kinapatikana katika viganja, mnapotuzuia tusiingie na hivi vyombo vya kielektoniki Mhe. Spika, inakuwa shida kwa sababu mtu unataka ku-*search* kitu huwezi. Kwa hiyo, kuturuhusu kuingia na hizi *electronic devices* mumetusaidia sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufanya *research* hata hapa hapa juu ya kiti wakati Mjumbe akiwa amekaa.

Lakini pia Mhe. Spika, niipongeze hatua hii kwa sababu hivi sasa dunia inabadilika, na kila kitu kinaelekea kwenye mambo ya teknolojia, kuna mambo ya *electronics;* siku hizi kuna *e- health, e- learning*, kuna *e- payment,* hata juzi Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania limepokea wafadhili kupitia mradi wa *LSP* kwamba hivi sasa linataka kuelekea katika *e- Parliament***.** Kwa hiyo, ingekuwa *awkward* sana wakati watu wanaelekea kwenye *e- Parliament* nyinyi mnazuia watu kuingia na *devices* kwenye Baraza. Kwa hiyo, nishukuru hatua hii kwamba mumeturuhusu na tunaamini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watatumia fursa hii uzuri ili kufanya *research* katika mambo ambayo wana-*present* hapa, kwa vile kila siku tunaambiwa kwamba tuseme yale ambayo tuna hakika nayo.

Jengine Mhe. Spika, naunga mkono kifungu cha 84(8) ambacho kinaruhusu Wajumbe ambao watakuwa wanapingana na mawazo ya kamati ya ujumla wataruhusika angalau Mwenyekiti aandike yale majina ya Wajumbe ambao hawakubaliani na yale mawazo. Kwa sababu mawazo Mhe. Spika, hatuwezi sote tukawa tunaenda kama nyumbu, sote tunaelekea upande mmoja kama wale wenzetu.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba demokrasia inasema wengi wape lakini wachache wasikilizwe. Kwa hiyo, hii itawapa fursa wale wachache ambao hawakubaliani na maoni ya kamati ya wengi angalau kupata kusikilizwa katika Baraza kupitia muwasilishaji wa hotuba.

Jengine Mhe. Spika, naomba nisisitize katika kanuni ya 96(3) ambayo inasisitiza serikali kuleta taarifa ama hotuba zile ambazo Wawakilishi wanatakiwa kuzichangia siku mbili kabla ya siku ya majadiliano.

Naomba serikali katika hili iwe makini sana kwa sababu nitatoa mfano juzi kulikuwa kunapitishwa Mswada wa *Procurement*.

Mhe. Spika, tumeletewa marekebisho ya *page* 27 asubuhi saa 3:00, niambie Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi anapata muda gani kutoka saa 3:00 mpaka saa 4:00 muda wa maswali unapoisha kupata kupitia marekebisho yale ili aje na

mapendekezo ama aje na mawazo ambayo atatoa kuishauri serikali au kupendekeza katika miswada ile.

Kwa hiyo, naomba lakini hata katika mambo ya tunapokwenda katika Bajeti unaletewa taarifa Mhe. Spika, imotomoto imetoka kwenye *photocopy* sasa hivi, yaani unaishika hivi imoto na *volume* kama hizi, nina uzoefu kabisa Wizara ya Idara Maalum, kwa hivyo munaishia kupiga juu kule ndani hamuingii vizuri na baadaye hapa kunapitishwa mambo baada ya siku mbili tatu utakuja kuona yanaleta matatizo.

Kwa hivyo, serikali ilivyosisitiza kwamba Wawakilishi wazingatie kanuni hizi na sisi tunawaambia wazingatie kanuni zile ambazo zinawahusu wao kutimiza wajibu wao. Taarifa za hotuba ikiwa za Bajeti ikiwa zozote ziletwe siku mbili kabla, ili Wajumbe wapate nafasi ya kusoma taarifa hizi na kuja na mawazo ambayo yatakayoweza kuisaidia serikali.

Jengine ambalo lilileta utata Mhe. Spika, katika kamati kulikuwa na mjadala mkubwa kuhusu hizi kamati za kudumu ni zipi na zile kamati nyengine zinakuwaje. Kwa sababu na mpaka tunamaliza kikao kile hatukupata ufafanuzi ipi Kamati ya Kudumu na nadhani hata hotuba ya Mwenyekiti imesema hapa ipi inakuwa kamati ya kudumu na ipi inakuwa kamati ambayo ni ya muda, na ni sifa zipi zinaipa kamati kuwa kamati ya kudumu tukawa tunajiuliza hivi ni kwa sababu imetajwa tu katika kanuni au ni ule muda ambao kamati inafanya kazi ndio inaiainisha hii kamati kama ya kudumu au ni kamati nyengine.

Kwa mfano Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe imetajwa kuwa ni kamati ya kudumu, lakini kamati hii sijui kama ipo, maana naona mpaka inaporwa mamlaka yake. Kamati hii inakuwa inafanya kazi za muda lakini katika kanuni imetajwa kuwa kamati ya kudumu. Kwa hiyo, mjadala ukawa mkubwa na naomba Mhe. Waziri akija hapa labda atufafanulie zipi zinakuwa Kamati za Kudumu na zipi zinakuwa kamati za kawaida.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niingie kwenye suala la jinsia. Nashukuru sana serikali lakini pia na kamati kwa kupendekeza kwamba pale ambapo chaguzi za kamati zitafanyika na kama hakutokuwa na Mwenyekiti wa Kamati mwanamke ambaye amechaguliwa, Serikali ilipendekeza kwamba Wawakilishi wanawake wakae kitako wachague wanawake wawili ambao watawakilisha wanawake katika Kamati ya Uongozi. Lakini sisi kama Kamati tukaona busara itumike, kwa sababu tumeshafeli tayari kuchaguana katika hizi Kamati za kawaida, tukaona bora busara itumike Spika achague wanawake wawili ambao watawawakilisha wanawake katika Kamati ya Uongozi.

Na lengo ni kwamba tumependekeza Spika apendekeze kwa sababu lengo letu ni kupeleka wanawake ambao ni *competent* na ambao wanajielewa na ambao wakifika huko hawatoburuzwa. Kwa hivyo tukasema tumuombe Spika apendekeze ili wanawake hawa wateuliwe na Spika kuingia katika Kamati ya Uongozi. Naamini kwa busara za Spika atachagua wale ambao anahisi watamsaidia katika kutekeleza kazi zake.

Jengine Mhe. Spika, la uchokozi na hili naomba Wawakilishi wanawake waniunge mkono kwamba mimi binafsi nilipendekeza kwamba Kamati ya Ustawi wa Jamii iwe inaongozwa na Mwenyekiti mwanamke. Kwani sisi ndiyo tunaojua matatizo ya wanawake huko, lakini pia ni sisi sisi ambao tunajua matatizo ambayo yanawahusu watoto. Lakini ukizungumzia kuhusu ustawi wa jamii basi kwa mwanamke utakuwa umefika. Kwa hivyo, nilipendekeza kwamba Kamati ya Ustawi wa Jamii iwe inaongozwa na mwanamke, na pengine isibadilike hivi sasa lakini baadae huko mbele ije kuwa katika uchaguzi unaofuata labda tuje kufikiria hilo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, naona umewasha *microphone* yako, ninakushukuru nina mengi lakini kwa hapa nilipofikia nawaachia Wajumbe wenzangu watayasemea yale mengine ambayo yamebakia.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe.Wanu Hafidh Ameir kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ajiandae.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe mukumbuke kwamba tulifanya semina kuhusiana na masuala haya. Kwa hivyo, sitegemei kwamba mutakuwa na michango mirefu sana kwenye hili, ili tuweze kufikia mwisho wa hili Azimio.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuwa mtu wa pili kuchangia alau kidogo katika marekebisho haya ya Kanuni.

Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na afya njema, na pia nchi yetu kuwa ni salama ili tukaweza kujadili mambo yetu humu katika Baraza. Hii ni neema kubwa sana.

La pili katika marekebisho haya mimi nitagusa sehemu tatu tu na kama ulivyokwishaeleza kwamba mengi tumeshasikia kwenye semina, lakini pia hapa ni sehemu muafaka napo kutia neno lolote.

Katika marekebisho haya Mhe. Spika, mimi kila nikikaa naona bado sijakaliwa vizuri na marekebisho haya yanayozungumzia masuala ya hii tafsiri neno "mgeni".

Kama alivyoelezwa mgeni hapa naomba ninukuu kwamba, Mgeni ni mtu yeyote ambaye si mwananchi, si Rais wa Zanzibar, si Spika au Mjumbe au Katibu, Mtumishi wa Baraza na kadhalika. Lakini hapa alipozugumzwa mgeni si mwananchi, mwananchi kama yupi hapa aliyezungumziwa naomba tafsiri zaidi nipate hapa ili na mimi kichwa changu kikae vizuri niweze kuelewa katika Kanuni hii.

Sehemu ambayo nyengine ambayo mimi nitachangia moja kwa moja niende kwenye marekebisho ya Kanuni ya 74. Kanuni ya 74 ya marekebisho mpya kwenye mahudhurio. Hapa imezungumzwa kwamba mahudhurio, kama mtu ambapo hatohudhuria kwenye Kikao cha Baraza au Kamati, alete taarifa kwa maandishi.

Lakini ikimbukwe kwamba kuna wakati mwengine maandishi, hiyo dharura itakukuta wapi, hiyo dharura itakukuta wakati gani. Kwa hivyo naomba kwamba vile tulivyo tujali katika kifungu hichi kilichotokea nyuma cha 78 kwamba kuruhusu kutumika elektroniki, basi elektroniki hii ya simu nayo ikubalike. Pale ambapo Mjumbe atakuwa na dharura ama iwe kwenye Kamati au kwenye Baraza, basi ikubalike kwamba ama kama atampigia Spika, kama hakumpata Spika basi Naibu Spika nayo ikubalike katika marekebisho haya, ili na yule Mjumbe aweze kupata ruhusa ya kuweza kuitumia dharura ile.

Pia Mhe. Spika, katika mahudhurio haya haya ambayo tunasema kwenye kudhibiti mahudhurio ambayo ndiyo uhai wa Baraza hili, kuchunguza mahudhurio na ndiyo uhalali wa vikao vyetu vyote vinavyokaa humu basi pamoja na kwamba tutasema Wajumbe wafanye mahudhurio asubuhi na jioni, lakini bado dawa naona haijakuwa rasmi. Kwani kuna Wajumbe baadhi yao wataitumia fursa hii vibaya, asubuhi ataweza kuja kuandika hapa na jioni atakuja, halafu baadae akafanye shughuli zake.

Ukiangalia wengine humu wanaganda katika viti kwa kuwa wanajua ndiyo wajibu wao uliowaleta hapa mpaka mwisho wa muda ambao umekubalika. Na tayari Baraza hili mimi ninaona linakwenda hivyo kwamba kuna Wajumbe

hawayatimizi majukumu haya. Wanakuja au pengine Mjumbe anakuja kwa siku ambayo anakuwa na hoja yake au ana swali lake.

Kwa hivyo, watu kama hawa tukiwapa fursa kama hii pia wataitumia vibaya. Naomba sana Baraza na Kanuni hii iangaliwe. Wale watakaokuwa wasimmizi basi waangaliwe watu kama hawa. Je, mwenendo wao vipi, isiwe ni kusaini asubuhi na jioni tu imetosha na kuweza kupata posho hili. Mtu kama huyu ikiwa ana shughuli zake ni bora aamue hili jimbo kuliacha na wengine wapo wanalisubiri wataweza kujaza nafasi hiyo, waje washughulikie wananchi hapa. Kwa sababu Wawakilishi hapa ndiyo wanaowasemea wananchi ambao kule hawana nafasi ya kuja kuzungumzia hapa.

Mhe. Spika, niende katika suala jengine ambalo kuwa ni suala la Taarifa ya Baraza. Kwa kweli Mhe. Spika, tunapata tabu sana tunapoona kwamba mambo yanakuja haraka haraka na halafu tunatakiwa kuyajadili, kama Miswada inavyoletwa. Inaweza ikaletwa Miswada mitatu au minne kwa siku moja na siku ya pili unaanza kujadiliwa na baadae unatakiwa upitishwe.

Miswada hii kwa mujibu wa taratibu inatakiwa ipelekwe kwa wananchi na wao angalau waijue, siyo wananchi wote ambao wataweza kuchangia, lakini ukipata fursa Miswada kama hii unapata kuipeleka kwa wananchi ambao wanaweza kuchangia lolote na baadae ukija hapa ukatoa mchango wako.

Kwani mtindo huu ambao unaendelea kutumika kuletewa Mswada baada ya siku moja au siku ya pili ukaanza kujadiliwa, hujapata kutoka na wengine majimbo yetu yapo mbali, itakuwa kwa kweli tunanyimwa fursa kama hii. Naomba sana suala hili liangaliwe la Miswada ambayo inaletwa Barazani.

Vile vile majibu ya Serikali, Kanuni inasema iletwe mapema pia vile vile majibu ya Hesabu za Serikali kutokana na Mawizara au Mashirika ya Umma yanatakiwa yalete mapema. Leo unafika asubuhi munakwenda kwenye Wizara au Shirika unakuta unaletewa ndiyo kama hivyo kopi bado ina moto wa mashine. Utakwenda kujadili nini, utakwenda kuhoji kitu gani. Kwa hivyo hili ni suala litolewe vizuri na kwa wale ambao watakiuka utaratibu huu wachukuliwe hatua. Kwa sababu inagharimu Baraza, inagharimu muda wa Wajumbe, kwa sababu inalazimika pengine kufika kule na kupika ripoti na kugeuka nyuma, hawawezi kujadili lolote kutokana na jambo lile ambalo wanalifuatilia. Kwa hivyo ni vyema sana uangaliwe kwa yule ambaye atachelewa kuleta majibu ya hoja kama hizo zinazohitajika, basi atachukuliwa hatua na hii itakuwa ni funzo kwa wengine.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni huo naomba tuendelee na ninashukuru sana kwa kunipa muda wako huo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na Mhe. Viwe Khamis Aballa ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia machache yanayohusiana na marekebisho ya Kanuni zetu hizi za Baraza.

Awali nimshukuru na nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamo wa Pili wa Rais kwa kuweza kuwasilisha hotuba yake juu ya marekebisho ya Kanuni hizi kwa ufasaha mkubwa. Lakini vile vile nichukue fursa hii ya kumpongeza au kuipongeza Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa ripoti yao ya marekebisho.

Nichukue fursa hii kumpongeza sana muwasilishaji Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, Mwakilishi makini wa Jimbo la Chaani kwa ufasaha wake wa uwasilishaji. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nina machache sana katika marekebisho ya Kanuni hizi. Nianze moja kwa moja bila ya kupoteza wakati katika ukurasa wa 17. Katika ukurara wa 17 Mhe. Spika, kwenye Kanuni inayohusiana na Miswada kuna Miswada ya Kamati ambayo imeongezwa hapa, awali ambayo ilikuwa haipo. Lakini vile vile kuna Mswada wa Mjumbe katika Kanuni ambayo inarekebishwa.

Mhe. Spika, suala la kuandaa Miswada ni suala ambalo linataka utaalamu. Ningependa tu nitoe ombi langu ili Wajumbe wa Baraza hili waweze kupata uelewa mkubwa sana juu ya taaluma ya kuweza kuandaa ule Mswada wa Mjumbe, lakini vile vile hii Miswada ya Kamati, ili kuweza kuona kwamba wanakuwa na uwezo lakini inapotokezea fursa basi waweze kuandika hiyo Miswada na kuiwasilisha katika Baraza.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 19 fasili mpya ambayo inayohusiana na utaratibu wa Mjumbe kuwasilisha Mswada ili kupata maoni ya wananchi.

Mhe. Spika, suala hili linawezekana linafanywa, inawezekana halifanywi. Na kama linafanywa pengine linafanywa kwa kiwango kidogo na Wajumbe na inawezekana kutokana na vile vile na ukosefu wa taaluma na utaratibu wa jinsi ya kuweza kupata maoni ya wananchi juu ya suala zima la kuchangia Miswada ambayo pengine moja kwa moja inawahusu.

Ningependa sana Baraza lichukue fursa hii ya kuweza kutoa taaluma vile vile kwa Wajumbe juu ya utaratibu mzuri wa kuweza Wajumbe kuweza kuitumia Miswada yao au Miswada yetu kuiwasilisha kwa wananchi ili hatimaye kuweza kupata maoni yao juu ya mambo yanayowahusu. Vile vile hili litatupa fursa hata sisi Waheshimiwa Wajumbe pale tunapozungumza au tunapochangia hii Miswada kupata ule uhalali wa kuweza kusema kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo fulani. Kwa sababu itakuwa umeweza kutenda haki katika hilo.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 39, kuna Kifungu kinachorekebishwa cha Kanuni 98 (6)(b), kuna neno shilingi moja. Katika marekebisho imesemwa kwamba itaandikwa upya kama ifuatavyo kwa kupunguza kiasi fulani cha fedha, yaani kuifuta shilingi moja na kuweka kifungu hicho kiasi fulani cha fedha. Lakini kwenye ukurasa wa 39 kwenye kipengele hichi cha huku kwenye marekebisho hili neno limejitokeza tena, upungufu wa shilingi moja. Sasa sijui huku, huku tumefuta lakini huku ile shilingi moja ninaiona tena. Sasa ningependa ufafanuzi kwa nini ikaingia tena.

Mhe. Spika, nikija katika ukurasa wa 47 Kifungu cha Kanuni 109 kwenye Kifungu cha (f), pana fasili mpya ya 109 (6) kama ifuatavyo, inasema "Endapo itatokezea Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza wote ni wanaume, Wajumbe wanawake watateua Wajumbe wawili miongoni mwao kuwa Wajumbe wa Kamati ya Uongozi.

Wenzagu hususan Mhe. Wanu Hafidh Ameir amelichangia hilo lakini mimi siendi katika upande huo. Ninaelewa kwamba katika Kamati hizi za Kudumu kuna Wajumbe wanawake ambao kutokana na nafasi zao hawaingii katika Kamati hizi. Kwa Baraza letu hili nina imani kwamba Naibu Spika haingii katika Kamati za Kudumu, lakini na Mawaziri hawaingii moja kwa moja katika Kamati za Kudumu, Mawaziri wanawake katika hili.

Sasa ningependa hapo isomeke kwamba Wajumbe wanawake wa Kamati za Kudumu za Baraza, ninarudia isomeke endapo itatokezea Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza wote ni wanaume, Wajumbe wanawake wa Kamati za Kudumu za Baraza, yaani wale tu ambao wamo katika Kamati za Kudumu za Baraza ndiyo watakuwa na fursa hii ninafikiri. Kwa hivyo hicho kipengele

kiwepo, "Wajumbe wanawake wa Kamati za Kudumu za Baraza", kiingie hapo hicho kipengele ili kuweza kuwatenga wale ambao hawana sifa za kuweza kuingia hapo. Ninafikiria inaweza ikakaa vizuri zaidi.

Lakini tukija katika ukurasa wa 52. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 52 kuna Kanuni mpya hii ya Bunge la Vijana. Hapa kidogo nilikuwa na pendekezo kwa sababu suala la Mabaraza ya Vijana yameanza katika ngazi ya Shehia, yakaja katika ngazi ya Wilaya, ninafikiri Mkoa na hatimaye Taifa. Neno hili huko nyuma linaeleweka Baraza la Vijana. Sasa hapa nilikuwa mimi ninapendeza baada ya kuwa na Bunge la Vijana, iwe ni Baraza la Wawakilishi la Vijana kutokana na maumbile ya hili neno tokea huko nyuma linakotoka.

Lakini nilikuwa na swali hapa Mhe. Spika, na Mhe. Waziri atakapokuja anaweza kutujibu kwamba hili Bunge au Baraza la Wawakilishi la Vijana kama ninavyopendekeza litakuwa na Kanuni zake nalo, na kama itakuwa na Kanuni zake basi ningependa nipate jawabu kwa sababu hapa limechukua nafasi ndogo tu kama Kanuni katika kulitambulisha.

Mhe. Spika, nimalizie tu kwenye ukurasa wa 53 katika Kanuni ya 160. Katika marekebisho, hii ni Kanuni mpya ninafikiri, "Haki ya Raia kujitetea na kujisafisha". Imeelezwa hapo katika *column* hiyo ya kulia kwamba mtu, "Mtu yeyote asiyekuwa Mjumbe ambaye atajisikia kuwa amepata athari...", inaendelea.

Mimi ninapendekeza hilo neno, "Mtu" hapo liondoke na lije neno, "Raia". Kwa sababu katika nchi yetu kuna watu wengi ambao siyo raia lakini Kanuni hii ninafikiri lengo zaidi ni kuwalenga raia wa nchi hii. Kwa hivyo baada ya kuweka neno "Mtu" ambalo lipo *very general*, basi tuweke "Raia" ambaye tunampa fursa hiyo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi nishukuru na ninaunga mkono marekebisho ya Kanuni hii asilimia mia kwa mia.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi. Sasa ninamwita Mhe. Mohamed Ahmada Salum Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo katika tokeo hili muhimu la kurekebisha Kanuni yetu hii ya 2012.

Na mimi sitokuwa na mengi ya kuzungumza isipokuwa nilikuwa na machache tu. Tukianza katika ukurasa wa mwanzo huu, mimi nilikuwa kidogo katika tafsiri ya mgeni. Sasa mimi nitakuwa na mapendekezo katika kusema maana yake ni mwananchi yeyote ambaye sio Rais wa Zanzibar, Spika, mpaka mwisho wa ibara hiyo.

Baada ya hapo nitakuja moja kwa moja mpaka ukurasa wa 37, kuhusu kanuni hii mpya ya 96(5). Mwisho kabisa katika marekebisho haya ya kanuni hii mpya, naomba muda usiozidi dakika 45 ubadilike na badala yake isomeke ibara hii ya 96(5) kama ifuatavyo.

"Baada ya majadiliano kumalizika, waziri anayehusika na uwasilishaji wa hotuba ya majadiliano yake, atapewa nafasi ya kujibu hoja inayotokana na michango ya wajumbe kwa muda usiozidi saa moja, na Spika, akiona inafaa anaweza kumuongezea waziri husika dakika zisizozidi 15"

Baada ya mapendekezo yangu hayo machache, na mimi nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja hii, na ninawaomba na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tukubaliane na marekebisho hayo ya kanuni ili tupate kwenda na wakati. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Naomba sasa nimwite Mhe. Viwe Khamis Abdalla, ili na yeye atoe mchango wake.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi fursa hii nikaweza kuchangia marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa uwasilishaji wake mzuri wa taarifa hii ya kanuni. Pia nimpongeze Mhe. Nadir Abdul-Latif kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria kwa uwasilishaji wake mzuri wa ripoti ya kamati.

Mhe. Spika, nianze mchango wangu katika ukurasa wa 14 kifungu cha 74 cha marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

"Endapo Mjumbe yeyote atakayehudhuria katika kikao cha asubuhi na kukosa kuhudhuria katika kikao cha jioni, basi atalazimika kukatwa posho".

Mhe. Spika, tutambue kwamba sisi ni Wawakilishi wa wananchi na tupo hapa tunawawakilisha wananchi. Wenzetu Wabunge wao hili posho lao limefafanuliwa. Kuna posho ambalo ni la kujikimu.

Kwa mfano, kama sisi ambao tunatoka Pemba kunakuwa na posho maalumu ambalo munapewa la kujikimu la kuwafanya mkaweza kuishi hapa Zanzibar. Pia kuna posho ambalo kama hukuingia kwenye vikao, basi posho lile hutoweza kupatiwa. Sasa namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atufafanulie. Posho hili ambalo tunalipwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza litakuwa linalipwa vipi, kwa sababu ni tofauti na wenzetu Wabunge wanavyolipwa posho hili, na sisi ni Wawakilishi wa wananchi na Waheshimiwa Wajumbe wanakuwa na dharura tofauti, tukiangalia na siasa sasa hivi inavyokwenda hapa Zanzibar. Sio kweli kwamba Mhe. Mwakilishi hatofiliwa jimboni kwake akaweza kuhudhuria katika kikao, ni lazima kwanza atakwenda kwenye mazishi na baadae atakuja kwenye kikao.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni huo, naomba tupatiwe ufafanuzi wa kutosha, yaani hizi posho tupatiwe ufafanuzi wa kutosha, ili na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tusije tukawa tunapitisha kanuni hizi ikawa zinatubana sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hao walikuwa ndio wachangiaji wetu. Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii sasa nimwite tena Mhe. Waziri ili sasa aje atoe ufafanuzi kwa yale ambayo yamejitokeza. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nichukue fursa hii niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kiasi kikubwa kuridhia kanuni zetu.

Kwa kuwa ni kanuni zetu hoja zao walizozitoa ni kwa ajili ya kufanya marekebisho ya hapa na pale, ambayo kimsingi ukiyatazama yanaendana na asili ya kanuni zenyewe. Kwa hivyo, marekebisho yenyewe waliyoyafanya Mhe. Spika, sio makubwa na ninaamini wakati wa kanuni wataalamu wetu wapo hapa kuna mambo ya msingi watayazingatia, na yale ambayo wanaona itabidi yabaki kama yalivyo, basi tutawaruhusu wafanye hivyo.

Mhe. Spika, hoja hii ilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe wafuatao. Naomba niwatambue kwa ruhusa yako.

1. Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf, kwa niaba ya Kamati
2. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, mwanangu. Ni mwanangu kwa maana ndani ya Baraza.
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Rashid Makame Shamsi
5. Mhe. Mohammed Ahmada Salum
6. Mhe. Viwe Khamis Abdalla

Mhe. Spika, hao ndio walikuwa wachangiaji wetu kwenye hoja hii ya kanuni. Naamini kwa sababu wengi tayari walishachangia kwenye semina, na kwa sababu waliona kila ambalo lililetwa wakati huo na tukalirekebisha limechukuliwa kwenye marekebisho, kwa hivyo ndio maana wachangiaji wakawa hawa waliojitokeza.

Mhe. Spika, kuhusu kanuni ya 74(3) kwa ajili wajumbe kukatwa posho pale inapotokea dharura, na hasa hasa Waheshimiwa Wawakilishi Wabunge wanaokwenda kwenye vikao vya Bunge.

Hakuna haja ya kuongeza kanuni nyengine, kwa sababu tayari kanuni ya 74(3)(c) inaeleza vizuri, kwamba itakapotokea dharura basi Kamati ya Uongozi itatoa muongozo wa dharura, likiwemo suala zima la Waheshimiwa Wawakilishi Wabunge wanaokwenda Bungeni. Hiyo itakuwa ni dharura wanapokwenda Bungeni, lakini isijekuwa Mheshimiwa anasema anakwenda Bungeni, kumbe yuko Paje. Hapo ni tatizo kidogo, au yuko Mfenesini, itakuwa bado hukuhudhuria kwenye Baraza la Wawakilishi na wala hukuhudhuria Bungeni pia. Kwa hivyo, suala hilo Kamati ya Uongozi italijua, kwa msingi huo bado msimamo uko pale pale. *(Makofi)*

Suala hili lilizungumzwa pia na Mhe. Viwe Khamis Abdalla, alilizungumzia hivi mwisho, kwamba inapotokezea dharura ya jimboni kwake Mjumbe, Mjumbe amefiwa na kadhalika.

Mhe. Mjumbe kama hukufuata taratibu za kanuni hizi, basi utakatwa posho, ukifuata taratibu za kanuni hizi na ukapata ruhusa kwa mujibu wa kanuni, basi posho halitokatwa. Hayo ndio makubaliano yetu, hii inaweka *commitment* na *seriousness* ya kuhudhuria kwenye vikao. Tunashindwa wakati mwengine kufanya maamuzi ya msingi kwa ajili ya *quorum*. Jana hapa ilibidi tubadilishe

utaratibu wa *order paper* kwa sababu ya *quorum,* na tukasimamisha kufanya uchaguzi wetu mpaka baadae tulipotimia.

Kwa hivyo, sisi ni watu wazima, tumepewa heshima kubwa ya kuwatumikia wananchi, wanataka waone *commitment* yetu na *seriousness* yetu katika kufanya mambo. Kwa hivyo, mimi naamini utaratibu uliopo wa kikanuni wa sasa utasaidia kufanya shughuli zetu vizuri, ili kuepukana na utoro. Maana haitakuwa heshima unakuja hapa unatangazwa Mhe. Mjumbe fulani mtoro sio jambo zuri hata kidogo, naamini iwe hivyo. Hata Mhe. Shehe Hamad Mattar alizungumzia hili suala. Akasema usijekuwa unasaini halafu umetoka unakuja tena kusaini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mtu uliyeaminiwa na wananchi kuja kuwawakilisha katika chombo hiki ni fursa ya kipekee. Hivyo, ujue kwamba wananchi wanakuona, wewe unaingia kwa saini sio kwenda kuwafanyia kazi zao, matokeo yake watakuacha njiani.

Vile vile, humu ndani tutakuwa na utaratibu wa kupeleka taarifa hizo kwa chama husika, msingi wake chama kitakuona wewe Mwakilishi mtoro hufai. Kwa hivyo, kitamuondosha kwenye nafasi hiyo ili kuweka heshima ya chama, kuweka heshima ya wananchi, ili mambo yaende vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Shehe Mattar suala hili lisikutie wasi wasi, kwa yule Mjumbe ambaye hatohudhuria anakuja humu kutia saini, tutajua huyu ni mtia saini, tutamuita hasa mtia saini, hafai huyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu Kamati ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Wanu Hafidh Ameir alipendekeza kwamba hii ipewe heshima maalumu kwa wanawake. Tatizo hapa kidogo napata tabu, kwa sababu ustawi wa jamii sio wa wanawake peke yao, ni wa wanawake na wanaume. Sasa na sisi pia wanaume tunautaka huo ustawi wa jamii. Sasa hivi tutakuwa tunaanza kutengana na sivyo hivyo. Kwa hivyo, tumtafute mwenye sifa na aliyekamilika achaguliwe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, akijitokeza mwanamama *smart* na mambo mazuri tunamchagua, akijitokeza baba *smart* na mambo mazuri kama Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) tunamchagua. Kwa hivyo, hapa muhimu iwe ni sifa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini liko jambo moja limejitokeza hapa na alituandikia Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kama mchango wake, akasema jambo moja hili linapotokea Mkuu wa Shughuli za Serikali ametokewa na dharura kubwa siku ya kuahirisha Baraza, tunafanyaje kwenye kanuni zetu.

Basi baada ya kushauriana na Mhe. Mwanasheria Mkuu pale, akasema tuchukulie utaratibu wetu huu tunaoufanya siku zote, anapokuwa Mhe. Makamo wa Pili wa Rais hayupo, basi waziri muhusika anayesimamia shughuli za Baraza afanye hiyo kazi kwa niaba ya Mkuu wa Shughuli za Baraza, ama mtu mwengine yeyote atakayependekezwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais kwamba akafanye kazi hiyo, nadhani itatusaidia kwenye msingi huo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu mafunzo ili kuelewa miswada. Ushauri huu umetolewa na Mhe. Rashid Makame. Siku zote Mhe. Rashid anapotoa michango yake hapa inakuwa ni ya kusisimua sana, ina uzito na inaonekana Mhe. Rashid Makame anafanya kazi sana ya kusoma, kujifunza na kupitia mambo. Hongera sana Mhe. Rashid Makame.

Mimi nafikiri hili ni jambo zuri, michango yako inatoa muelekeo mkubwa katika kuimarisha chombo hiki. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu suala la shilingi moja imejitokeza tena. Mimi nadhani hoja hii tuwaachie waandishi wetu wa kanuni, wao wataliweka katika utaratibu mzuri wa mtiririko unaofaa ambao hautatuletea migongano humu ndani. Tuwaachie wao na tuwaamini na nia yao ni kufanya kazi vizuri.

Mhe. Spika, kuhusu hili suala la marekebisho ya kuingiza wajumbe wanawake, pale ambapo imetokea pengine wajumbe wengi wamekuwa wanaume.

Mimi nadhani ulitoa ushauri kwamba ionekane neno wajumbe waliomo kwenye kamati za kudumu. Nafikiri sio neno baya, maana yake itakuwa hakuna aliyekuwa kwenye kamati za kudumu katika Mjumbe wa Baraza. Kwa hivyo, nadhani ni ushauri mzuri wenzetu katika uandishi wataliwekea utaratibu mzuri ili liweze kufanya kazi.

Mhe. Spika, hii hoja ya kusema Baraza la Wawakilishi, badala ya Bunge la Vijana. Nafikiri kwa maana ya kusema Baraza la Wawakilishi la Vijana, kwa sababu kuna chombo cha Baraza la Wawakilishi, hiyo ni hoja sahihi na yale mengine yanajieleza yenyewe ndani ya kanuni. Kwa hivyo, tuiwachie kanuni yetu haya watayapitia wataalamu wetu hapa yaende vizuri, ili tuwe na kanuni zilizo barabara.

Mhe. Spika, kuhusu mambo ya tafsiri. Mimi nadhani kwa kuwa suala la tafsiri ni la kitaalamu zaidi, kama kuna tafsiri yoyote ambayo imekwenda kinyume na utaratibu wa kanuni zetu ama inagongana na utaratibu wowote wa kisheria na kikatiba, tunaomba wataalamu watutizamie, ili kanuni inapokuja hapa, kabla ya

kuanza kuitumia tutaipitisha sote kwa pamoja tena, tutaitizama na tukiona imekamilika ndio itafanya kazi. Kuliko kuingilia sana tufanye hivi na vile, ikawa ule mtiririko wa uandishi ukatuletea matatizo mwisho wa siku. Mimi naona hilo ni sawa.

Vile vile Mhe. Spika, ipo hoja ya muda. Hoja hii tumeizungumza sana na hapa inabidi tukubaliane, kwa sababu tukipata ushauri pale muda wa kuwasilishia unakuwa mkubwa kuliko muda wa kufanya majumuisho.

Kuna hoja kwamba muda wa kufanya majumuisho unatakiwa nao uwe mkubwa ili kuelimisha wajumbe, nalo lina mtihani wake, na kuna wengine, kwa sababu humu ndani tumeshaona uzoefu, unaeleza kwa kina matokeo yake buti zinakurudia pale pale. Lakini kwa kweli wanapoelewa inakuwa vizuri hata buti zikijitokeza zina unafuu wake.

Mimi nadhani tufikie uamuzi mzuri kuhusu nini tufanye kwenye kuwasilisha na kwenye kufanya majumuisho, kwa sababu sikuipata ile mizania vizuri tufikie uamuzi gani. Mimi nadhani bado tukiwaachie kiti cha Spika. Basi nimepata ushauri mzuri iwe ni saa moja. Kwa hivyo, saa moja ni nzuri, nadhani tunakubaliana kwa pamoja, ahsante sana.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya malipo tutalipa vipi. Hii tumeshaieleza.

Basi baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, niseme kwamba niwashukuru tena Waheshimiwa Wajumbe kwa michango mizuri. Naamini tumekubaliana kuhusu hoja hii ya Kanuni.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Haya Mhe. Machano Othman Said.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, kwa kufanya majumuisho yake vizuri. Isipokuwa Mhe. Spika, utaratibu wangu ninaotaka kuzungumzia ni kwamba tulipokutana kwenye Kamati na hata kwenye semina, baada ya maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe kuhusu kukatwa posho asubuhi na jioni, na kwenye kamati tulianza na *per diem* na mambo mengine, tukakubaliana hili jambo liachwe kwenye mkono wa Spika, lisiwekwe moja kwa moja kwenye kamati, kwa sababu litaleta madhara makubwa kwa Baraza.

Baraza ni dogo na pato lao pia ni dogo kuliko Bunge, lakini pia ukiangalia Bunge wana *per diem* na wana *sitting*. Kwa hivyo, sisi tulikubaliana na kwa mazingira ya Zanzibar, kwanza tuache kama tulivyo sasa, ingawa kuandika mahudhurio ya asubuhi na jioni liendelee, lakini hayo mambo mengine yasiendelee, nilitaka kuweka sawa hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman. Nadhani serikali haionekani. Sijui Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, labda u-*respond* kwenye hili kidogo tu la Mhe. Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa sote ni wadau ushauri kama huu hakuna anayeweza kuukataa, ni ushauri mzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, hoja iliopo mbele yetu hapa ni Azimio la Marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, nawaomba sasa niwahoji. Wale wote ambao wanaunga mkono marekebisho hayo ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi wanyanyue mikono yao. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kura hiyo sasa marekebisho ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi yatakuwa yameshakuwa rasmi. Kwa hivyo, tutawaachia wanaohusika waweze kuweka pamoja, na baada ya hapo nafikiri tutapata vitabu vya kanuni mpya katika hizo siku za mbele za shughuli zetu.

Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamwita mtoa hoja ya kufunga, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, niwaite Mawaziri ili waje wasome Miswada yao kwa mara ya kwanza nianze na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Muswada wa Sheria ya Bendera ya Zanzibar, Nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya 2016

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Nembo N0.1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Bendera ya Zanzibar No.12 ya mwaka 2004 na Kutunga Sheria inayoweka Masharti bora yanayohusiana na bendera ya Zanzibar, nembo ya Serikali na Wimbo wa Taifa wa Zanzibar ya mwaka 2016 na Mambo yanayohusiana na hayo, kusomwa kwa mara ya kwanza.

Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako tena naomba nisome tena Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Tume ya Uchaguzi No.9 ya mwaka 1992 na kutunga Sheria ya kuanzisha Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Majukumu, Uwezo na mambo yanayohusiana na hayo kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2016

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Waziri wa Afya): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, dawa na Vipodozi No.2 ya mwaka 2006 kusomwa kwa mara ya kwanza.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ili aje atoe hoja yake ya kuahirisha.

KUAHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mwingi wa Rehma kwa kuendelea kuiweka nchi yetu hii katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa. Hali ambayo imeendelea kuipa nafasi Serikali na wananchi wa Zanzibar kuzidi kupata ufanisi wa shughuli zao za kila siku bila ya mtafaruku wa aina yoyote. Naendelea kuwasisitiza Viongozi pamoja na wananchi wote kwa jumla waendelee kushirikiana katika kuitunza na kuithamini amani iliopo nchini.

Mhe. Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kwa kutukutanisha hapa tukiwa katika hali ya uzima

na salama na kutuwezesha kufanikisha vizuri Mkutano wa Nne wa Baraza hili Tukufu la Tisa la Wawakilishi, ulioanza tarehe 23 Novemba, 2016. Kwa ujumla shughuli zote zilizopangwa katika ratiba ya Mkutano huu zimekamilika kwa wakati na kwa ufanisi.

Mhe. Spik**a,** napenda kutoa pongezi maalum kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuweka historia mpya katika nchi yetu kwa kusaini Sheria ya Utafutaji, Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia mbele ya kadamnasi ya watu hapo Ikulu. Sheria ambayo ilipitishwa na Baraza lako Tukufu la Wawakilishi, katika Mkutano wa Tatu. Itakumbukwa kuwa ahadi hii niliitoa Barazani hapa wakati naakhirisha Baraza la Tatu kwamba ningemuomba Mheshimiwa Rais kwa niaba yenu aisaini Sheria hiyo mbele ya wananchi na vyombo vya habari. Namshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kutukubalia ombi letu hilo.*(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake na kuhakikisha yanakwenda kwa ufanisi kwa kuwateua Viongozi kwenye Baraza na ndani ya Mawizara. Aidha, kwa niaba ya Baraza lako Tukufu nachukua fursa hii, kuwapongeza kwa dhati wale wote walioteuliwa kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Sira Ubwa Mamboya kuwa Mjumbe wa Baraza lako Tukufu.
2. Mhe. Mihayo Juma N'hunga kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.
3. Mhe. Shamata Shaame Khamis kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.
4. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman kuwa Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Tunawapongeza sana kwa kupata imani hii ya Mheshimiwa Rais. Tunamkaribisha sana Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya kwa mara nyengine hapa Barazani.*(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa pole kwa familia, Serikali na wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kwa kifo cha aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Sammuel Sita. Aidha, tunatoa pole kwa kifo cha Mbunge wa Jimbo la Dimani wa Chama cha Mapinduzi, Mhe. Hafidh Ali Tahir. Nawaomba wana familia na wananchi waendelee kuwa na subira katika misiba hii miwili mikubwa. Tuko pamoja nao katika kipindi hiki kigumu cha huzuni na maombolezo.

Mhe. Spika, naomba pia niwape pole wananchi wa Cuba kupitia Balozi wa Cuba nchini kwa kuondokewa na Kiongozi Jemedari wa nchi hiyo Marehemu Fidel Castro, ambaye alikuwa Kiongozi mahiri na mpigania uhuru na haki kwa nchi yake pia alikuwa mwana Mkombozi wa Bara la Afrika, Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi, Amin.

Mhe. Spika, katika kuendeleza uboreshaji wa Mji wa Zanzibar Serikali inaendelea kusimamia kuwepo kwa mandhari nzuri na haiba ya Mji wetu ambapo wafanya biashara wanaouza mbao katika eneo la Kijangwani, wameondolewa katika eneo hilo na Serikali imewaelekeza kuhamia katika eneo maalumu lililotengwa kwa ajili yao huko Darajabovu. Eneo la Kijangwani litafanyiwa marekebisho makubwa ya miundombinu ili liweze kutumika kama stendi ya magari.

Aidha, napenda kuwakumbusha wananchi kwamba zoezi hili ni endelevu ambalo litaendelea katika maeneo mengine ambayo wafanya biashara wameyavamia na kufanya biashara zao bila ya mpango maalum kama nilivyoeleza katika Hotuba ya Kuakhirisha Mkutano wa Tatu. Serikali inaendelea na mkakati wake wa kuufanya mji wa Zanzibar kuwa na haiba inayostahiki. Tunawaomba wananchi waendelee kuyaunga mkono mazoezi ya aina hii.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii, kulaani na kukemea tabia inayoonekana kukuwa ya udhalilishaji kwa watoto na wanawake, na hasa kulawitiwa kwa watoto wanaume. Naomba wenye tabia hizo waache mara moja kwani sio utamaduni wetu na wale watakaoendelea na tabia hiyo, naviomba vyombo vya sheria kuwashughulikia ipasavyo ili tabia hiyo iondoke nchini mwetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mnamo siku za hivi karibuni wananchi wengi wamepiga kelele sana kuhusu vilabu vya pombe kufunguliwa katika maeneo ya makaazi ya watu. Naomba kutoa wito kuwa vilabu hivyo na mabaa yasijengwe katika makaazi ya watu na pale ambapo kutakuwa na baa hizo, zifuate sheria zilivyo ili kulinda mila, utamaduni wa kutokuudhi watu ili kuimarisha heshima ya nchi yetu. Pia tudhibiti upigaji wa muziki katika maeneo ya makaazi kwani baadhi ya maeneo yamekuwa na kelele kubwa wakati wa usiku. Hatukatazi watu kufurahi na kusikiliza muziki lakini tuzingatie sheria na taratibu ambazo hazitosumbua watu wengine.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kwa niaba ya Baraza lako Tukufu kuendelea kuwapa pole sana wananchi wa Pwani Mchangani, Mkoa wa Kaskazini,

Unguja walioharibiwa vipando vyao. Pia, tunawapa pole Kikosi cha Vyuo vya Mafunzo kwa kuharibiwa mazao na vipando vyao katika shamba lao la Tungamaa, Pemba. Serikali itaendelea kudumisha amani na utulivu hivyo wale wote wavunjifu wa amani wataendelea kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Kwa mara nyengine tena nachukua nafasi hii, kuwataka wananchi waendelee kuwasihi vijana wao wasijiingize katika vitendo vya uvunjifu wa amani na vile vya ufisadi. Ninaviomba vyombo vya dola kuwachukulia hatua kali wale wote watakaovunja sheria na kuhatarisha amani na utulivu tulionao nchini.

Mhe. Spika, kama tujuavyo miezi michache iliyopita nchi yetu ilipata mripuko wa ugonjwa wa kipindupindu. Mripuko huo ulitokea mwezi Septemba mwaka jana hadi mwishoni mwa mwezi wa Julai mwaka huu. Baada ya hapo hali ya nchi yetu ikarejea katika hali yake ya kawaida hadi sasa. Lakini katika mripuko huo zaidi ya watu 4,330 waligundulika kuwa na ugonjwa huo, kati yao Unguja walikuwa 2,652 na Pemba ni 1,678.

Mikoa iliyoathirika zaidi ilikuwa Mjini na Magharibi kwa Unguja na Wilaya ya Micheweni kwa Pemba. Kwa bahati mbaya kati ya wagonjwa hao, wagonjwa 68 walifariki dunia (48 Unguja na 20 Pemba).

Mhe. Spika, mengi yamefanyika katika jitihada za kupambana na mripuko huu zikiwemo jitihada za wananchi wenyewe kuweka safi mazingira, kuimarisha usafi majumbani mwao na kufuata maelekezo yaliyokuwa yanatolewa na wataalam wa afya. Napenda kupongeza sana mashirikiano makubwa yaliyoonyeshwa baina ya Wizara ya Afya na Taasisi nyengine zinazohusika na udhibiti wa maradhi haya.

Mhe. Spika, napenda kuishukuru Wizara ya Afya, Ofisi ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya, *ZAWA*, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Vyombo vya Habari vya Serikali na vya watu binafsi ambavyo vilisaidia sana na kutoa elimu kwa wananchi. Niwapongeze wale wote waliotoa misaada ya hali na mali wakati wa harakati za kupambana na mripuko huu.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kutoa wito kwa wananchi, na wafanyabiashara na wahusika wa Taasisi zinazosimamia, kuendeleza utamaduni uliopo wa usafi na kutunza mazingira ili kuondokana na kuenea na kusambaa tena kwa maradhi ya kipindupindu. Itakumbukwa kuwa mara nyingi zinapoanza mvua maradhi haya hujitokeza. Hivyo, nawaomba wananchi kuendeleza usafi wa mazingira na nyumba zetu kwani kinga ni bora kuliko tiba.

Mhe. Spika, katika kikao hiki jumla ya maswali ya msingi thamanini na tano (85) na maswali ya nyongeza mia mbili na moja (201) yaliulizwa na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kutumia nafasi yao ya kuihoji Serikali pia natoa pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri kwa namna walivyojibu maswali hayo na kutoa ufafanuzi fasaha. Nawapongeza sana Mawaziri hao wote. Nawaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waendelee kuisimamia Serikali kwa kuihoji na kuikosoa kila wanapoona pana haja ya kufanya hivyo bila hofu wala woga, kwani kufanya hivyo kutaitanabahisha Serikali kutekeleza wajibu wake kwa usahihi zaidi.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani na pongezi maalum kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna anavyoisaidia Serikali katika kutoa ufafanuzi wa kisheria kila lilivyojitokeza jambo ambalo lingehitaji ufafanuzi wa kisheria, amefanya kazi kubwa na nzuri na ameonesha umahiri mkubwa katika fani yake ya sheria.

Mhe. Spika, katika mkutano huu, jumla ya Miswada Minne (4) imejadiliwa na kupitishwa kuwa Sheria na Baraza lako Tukufu. Miswada yenyewe ni:-

1. Mswada wa kwanza ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kutunga upya Sheria ya Ushahidi Sura ya Tano na Masuala Yanayohusiana nayo.

2. Mswada wa pili ulikuwa ni Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam. 2 ya 2005 Kuweka Masharti Bora zaidi kwa ajili ya Ufanisi na Usimamizi Imara wa Mfuko na Mambo yanayohusiana na Hayo.

3. Mswada wa tatu ulikuwa ni Mswada wa Sheria wa Kufuta Sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzishwa Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma na kuwekwa masharti mengine Yanayohusiana na Hayo, na

4. Mswada wa nne ulikuwa ni Mswada wa Sheria wa Kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kwa kuweka masharti bora ya kudhibiti na kusimamia fedha za umma na kuweka mambo mengine

Yanayohusiana na Hayo na kufuta Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Serikali Nam. 12 ya 2005.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba Miswada hiyo minne tuliyoipitisha itasaidia sana kwa kuweka misingi bora zaidi ya utendaji na pia kukuza uchumi wa Zanzibar. Ni dhahiri kwamba kupitishwa kwa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria na kutunga upya Sheria ya ushahidi Sura ya tano na masuala Yanayohusiana na Hayo, Sheria hii itasaidia sana kupunguza hadi kuondosha kabisa vitendo vya udhalilishaji nchini.

Naomba nichukue fursa hii kuwataka wananchi waendelee kutoa mashirikiano zaidi kwa Serikali na Taasisi zake katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Namba 2 ya mwaka 2005, kuweka masharti bora zaidi kwa ajili ya ufanisi na usimamizi imara zaidi wa Mfuko na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wameweza kuuchangia Mswada huu kwa kina, maoni na mapendekezo yao yamepokelewa na Serikali na yatafanyiwa kazi kwani marekebisho ya Sheria hii yamelenga zaidi kuwanufaisha wafanyakazi wakiwa kazini na baada ya kustaafu.

Mhe. Spika, katika Mkutano huu wa Nne Baraza lako Tukufu limepitisha Mswada wa Sheria wa Kufuta sheria ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Serikali Nam. 9 ya mwaka 2005 na Kutungwa Sheria inayoanzishwa Mamlaka ya Manunuzi na Uuzaji wa Mali za Umma na kuwekwa masharti mengine Yanayohusiana na Hayo, pamoja na Mswada wa Sheria wa Kutunga Sheria ya Usimamizi wa fedha za umma kwa kuweka masharti bora ya kudhibiti na kusimamia fedha za umma na kuweka mambo mengine Yanayohusiana na Hayo na kufuta sheria ya usimamizi wa fedha za Serikali Nam. 12 ya 2005. Kupitishwa kwa Miswada hii miwili kutaendelea kusimamia udhibiti wa mapato na kuendeleza nidhamu za matumizi ya fedha za umma. Sura ambayo inaelekea bayana kuendelea kuimarisha uchumi wa nchi hii. Naomba nitoe wito maalumu kwa Viongozi na Watendaji wa Serikali na Taasisi zake kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu na umakini zaidi.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru wale wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Nne wa Baraza la Tisa la Wawakilishi kwa ufanisi mkubwa.

Pongezi zaidi ziwafikie Watendaji wote wa Baraza hili la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu, Ndugu Raya Issa Msellem. Ni ukweli usiofichika

kwamba shughuli zilienda vizuri na ninaamini tutaendelea vizuri katika mikutano ijayo. Pia nawapongeza Wakalimani wetu wa lugha ya alama ambao wamewawezesha Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa jumla wenye ulemavu wa kusikia kufuatilia yote yaliyokuwa yakiendelea ndani ya Baraza. Vile vile, nawashukuru Wanahabari kwa kufanya kazi ya kuwahabarisha wananchi wetu yale yaliyokuwa yakiendelea Barazani hapa.

Mhe. Spika, pamoja na Miswada yote iliyopitishwa pia Baraza lako tukufu limepitisha marekebisho ya Kanuni za Baraza, najua kuwa kanuni hizo zitasaidia sana Baraza kufanya kazi zake vizuri zaidi na kwa umakini mkubwa zaidi.

Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sikukupongeza wewe, Mhe. Naibu Spika na Wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza vizuri na kwa ufanisi mkubwa Baraza hili. Hekima na busara zenu zimesaidia sana katika kuumaliza mkutano huu salama.

Mhe. Spika, kwa kumalizia niwatakie Waheshimiwa Wawakilishi kila la kheri na mafanikio mema katika kuwatumikia wananchi wao Majimboni mwao. Aidha, nawatakia safari njema na ya salama ya kurudi Majimboni mwao, na hasa Wawakilishi wenzetu kutoka Pemba kwa sababu wao wana safari ndefu zaidi kuliko wenzao wa Unguja.

Mhe. Spika, aidha, naomba kuchukua fursa hii kuwatakia Sikukuu Njema ya Maulid, Krismas Njema na nikupeni Heri ya Mwaka Mpya kwa vile sherehe hizi zote zipo muda mfupi kutoka sasa na zitafanyika kabla ya Mkutano wa Tano wa Baraza la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liahirishwe hadi siku ya Jumatano tarehe 15 Februari, 2017, saa 3.00 barabara za asubuhi panapo majaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa naomba niwahoji wale wote wnaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais ya kuahirisha hiki kikao mpaka ya Jumatano tarehe 15/02/2017 wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kufikiwa)

Waheshimiwa kabla sijaahirisha shughuli za Baraza nitoe matangazo machache yafuatayo:

1. Kukumbusheni kwamba kuanzia saa nane tutakuwa tuna semina hapa kama tulivyokuwa tumepanga jana, kwa hivyo tukimaliza shughuli za swala na chakula cha mchana tujitahidini sana kwa sababu tunategemea kuanza mapema sana saa 8.00.

2. Wajumbe wa Kamati Tendaji ya UWAWAZA mnaombwa kufika Ofisini kwa Naibu Spika, mara baada ya kuahirishwa mkutano.

3. Tangazo jengine ni la Wageni; ni Wageni wa Ofisi ya Makamuwa Pili wa Rais, Mgeni wa mwanzo ni Bi Khadija Naif, huyu ni *Presenter of Qatar Royal Family* na mmiliki wa *Naif Company Limited* karibu sana.*You're most welcome!*

4. Mgeni wetu wa pili ni Bi Zain Ahmed huyu ni mtayarishaji na mtangazaji wa kipindi cha *Profile* cha Channel Ten Dar es Salaam.

5. Mgeni wetu wa tatu ni Bw. Munir Zakariya huyu ni maarufu kwa hivyo yuko pamoja na hawa wageni wawili waliotangulia, karibuni sana Baraza la Wawakilishi.

6. Waheshimiwa Wajumbe pia mnatangaziwa kuwa katika mchezo wenu wa kesho Mgeni rasmi atakuwa ni Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Rashid Ali Juma.

Waheshimiwa mara baada ya kuahirisha hapa mtasimama kwa ajili ya wimbo wa taifa, na baada ya hapo ndio tutatoka, kwa hivyo nachukua nafasi hii kutangaza kuwa naahirisha shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka siku ya Jumatano tarehe 15/2/2017 saa .3.00 asubuhi.

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Wimbo wa Taifa uliimbwa kuashiria kuahirishwa kwa Mkutano)

(Saa 11.41jioni Baraza liliahirishwa hadi siku ya Jumatano tarehe 15/2/2017 saa 3.00 asubuhi)